# Nipashe

Alhamisi Januari 19, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581195

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT TZS. 1,067,615,605 KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




**Afariki** dunia kwa kuangukiwa na mti akimwokoa mwanawe

UKURASA 3




UKURASA 11

SAKATA LA KIMARO

# Wazee wa Kanisa sasa wawaangukia waumini

• **Mkuu** wa KKKT atoa kauli... *Ukurasa 2*



Askofu Dk. Fredrick Shoo



## 'Kichaka' cha uchakachuaji mbolea ruzuku chafichuliwa

UKURASA 3

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, akiangalia mifuko mitupu, mashine ya kushonea mifuko pamoja majenereta mawili baada ya kukamatwa mjini Njombe jana. **PICHA: ELIZA KILINDI**

## NBS yatangaza ahueni mfumuko wa bei kwa vyakula na vinywaji

UKURASA 2




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akizungumza na wawekezaji, wadau wa maendeleo pamoja baadhi ya viongozi wakuu wa nchi za Afrika katika Mkutano wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA) jijini Davos, Uswizi jana. **PICHA: IKULU**


**MICHEZO** NABI AISUKA UPYA SAFU YA USHAMBULIAJI UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Iringa (RTO), SP Mosi Ndozero, akitoa elimu ya usalama barabarani kwa madereva wanaoendesha magari kutoka bandarini kuelekea nchi jirani maarufu IT, katika Kituo Kikuu cha Polisi Mjini Iringa juzi. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Wazee wawaangukia waumini sakata la kuondolewa Kimaro

**Na Mary Geofrey**

SAKATA la Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Kijitonyama, Dk. Eliona Kimaro, limezidi kushika kasi huku waumini wa usharika huo wakizidi kuweka shinikizo la kutaka arejeshwe na kuendelea na huduma.

Wakati sakata hilo likiendelea, Wazee wa Kanisa katika usharika huo wamewaomba waumini kutokufanya mikusanyiko nje ya kanisa badala yake wakusanyike ndani ili kutoleta picha mbaya kwa kanisa.

Aidha, Mkuu wa KKKT, Dk. Fredrick Shoo, ametoa tamko kwamba waumini hao wanapaswa kuwa watulivu kwa wakati huu ambao suala hilo linashughulikiwa.

Dk. Kimaro alipewa likizo ya siku 60 na uongozi wa juu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP) na kwamba baada ya likizo hiyo, anatakiwa kuripoti makao makuu ya Dayosisi, Luther House, jijini Dar es Salaam.

Jana asubuhi, ikiwa ni siku moja baada ya waumini kukusanyika eneo la kanisa wakiwa na mabango, katika ibada, idadi ya waumini ilikuwa ya kuhesabu tofauti na ilivyozoeleka, huku baadhi ya waumini waliokuwa nje ya kanisa wakionyesha ishara ya kudai kurejeshwa kwa mchungaji wao. Jana waumini walioruhusiwa kushiriki ibada hiyo ni wale ambao uongozi wa usharika uliwahoji taarifa zao mlangoni kujua kama ni washirika. Baada ya ibada hiyo, Mzee wa Kanisa alitoa tangazo ibadani hapo kusema wanaungana na waumini wengine kuombea tukio la kusimamishwa kwa Mchungaji Kimaro.

Alisema baraza la wazee la usharika linashughulikia suala hilo kwa kushirikiana na mamlaka zingine zinazohusika na kuwasihi wawe watulivu kwa kuishi katika sala na toba.

"Mtu awaye yote asizuie masifu ya asubuhi wala masifu ya jioni wala ibada yoyote kwa sababu Mungu wetu ni wa utaratibu naye ametuwekea utaratibu. Msije mkadhani kwamba jambo hili halishughulikiwi. Wazee wenu wanalishughulikia kwa kushirikiana na mamlaka zote kuweka sawa," alisema.

Alisema wale waliochapisha fulana na ujumbe wa kwenye mabango zitumike kuingia kanisani ambako ni sehemu sahihi ya kuzungumzia na kuombea mambo yote badala ya nje ya kanisa.

"Mtu ana suala lake kuhusu suala hili, wote tukutane ndani ya nyumba ya ibada kwa ajili ya kuliombea ndipo Mungu atatujibu katika hema ya kukutania na wala usiandamane tukutane hapa, humu ndani ndio inaleta amani," alisema.

Alifafanua kuwa, yeyote atakayefanya kinyume na walioyaelekeza watamhesabia mtu kama anataka kutuletea fujo ambazo hatuzitaki na si utamaduni wao.

"Tuwe na utulivu na tuwe na subira. Katika kila jambo Mungu ana kusudi lake, hivyo tumpe Mungu nafasi, atatenda kwa wakati wake, niwashukuru wote mlioshukuru ibada ya asubuhi na wale mtakao kuja ile ya jioni. "Wapo wanaotutakia mema na wasiyotutakia mema yamkini nyie wacha Mungu mtakuwa na utulivu huo lakini watakuwapo wengine ambao watatumia fursa hii kufanya mambo ambayo siyo wasilichafue kanisa wasituchafue kwa maana lipo imara, tunaomba utulivu," alisisitiza.

**ASKOFU SHOO ATIA NENO**

Akizungumza na moja ya chombo cha habari juzi Mkuu wa KKKT, Dk. Fredrick Shoo, aliwaomba utulivu kwa washarika na wakristo ambao wamesikia habari za uamuzi uliofikiwa na dayosisi yake.

"Tutambue kuwa dayosisi ina vyombo vyake vya maamuzi na bila shaka jambo lenyewe linaendelea kufanyiwa kazi na dayosisi husika, baadaye sisi ambao tumepokea taarifa kama hizi tunaendelea kufuatilia na kupata taarifa zaidi kuhusu jambo hili ambalo linaonyesha limeleta usumbufu na mwitikio tofauti kutoka kwa watu wengi.

"Kubwa sana ambalo ningeomba wakristo hawa waumini wa usharika wake waweze kuwa watulivu wakati jambo hili linaendelea kufanyiwa kazi," alisisitiza Askofu Shoo.

# Samia ataka ushirikiano imara kushughulikia changamoto Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesisitiza umuhimu wa kuimarisha ushirikiano na wadau wa maendeleo katika kuzitafutia ufumbuzi changamoto za uwekezaji ili nchi za Afrika ziendelee kuzalisha kwa tija.

Alitoa rai hiyo jana wakati akizungumza na wawekezaji, wadau wa maendeleo pamoja na baadhi ya viongozi wakuu wa nchi za Afrika katika mkutano wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA), uliofanyika Davos nchini Uswizi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, katika mkutano huo mambo yaliyopewa kipaumbele kwenye mjadala huo ni sekta ya uzalishaji.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa katika mjadala ilionekana Bara la Afrika lina malighafi ya kutosha na zote hupelekwa nje ya nchi kwa uzalishaji na kwamba wametaka itafutwe namna ya kushirikiana kikamilifu kwa sekta ya umma, binafsi na wawekezaji kushirikiana ili uzalishaji wa bidhaa mbalimbali ufanyike ndani ya nchi husika. "Jambo jingine lililopendekezwa kwenye ukanda huo wa Afrika ni kuwapo na dira itakayokamilika siku za usoni za kuwapo mdhibiti wa bara zima badala ya kila nchi kuwa na mdhibiti wake hasa kwenye masuala ya biashara na dawa," alisema.

Aidha, wadau walishauri masuala ya nishati na kilimo kupewa umuhimu na serikali za nchi za Afrika, pamoja na kushirikiana katika mikakati endelevu kwa pamoja hali itayosaidia vijana wengi kupata ajira kupitia sekta hizo.

# NBS yatangaza ahueni mfumuko bei vyakula

**Na Restuta James**

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS), imetabiri kwamba mfumuko wa bei za bidhaa za vyakula na vinywaji baridi unatarajiwa kupungua kwa asilimia moja katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka huu.

Pia imesema mfumuko wa bei kwa ujumla unahimilika kwa kuwa bado uko kwenye tarakimu moja.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema hayo jijini Dar es Salaam, alipokuwa akifungua kikao kazi cha waandishi wa habari, ofisi ya takwimu na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Alisema ofisi hiyo imefanya maoteo ya mwenendo wa mfumuko wa bei za bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa Januari hadi Machi, ili kuisaidia serikali kufanya uamuzi wa kisera wenye vigezo vya takwimu.

"Maoteo hayo yanaonyesha mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi utaendelea kupungua kutoka asilimia 9.7 Desemba, mwaka jana, hadi asilimia 8.4 Machi, 2023," alisema.

"Tanzania itaendelea kuwa na mfumuko wa bei stahimilivu ndani ya kipindi cha robo mwaka ya kwanza ya mwaka 2023. Hadi kufikia Machi, baadhi ya maeneo nchini yatakuwa yameanza mavuno ya mazao, hivyo kupunguza shinikizo la bei lililoko sokoni," alisisitiza.

Dk. Chuwa alisema mikakati ya serikali ya kudhibiti upandaji wa nishati kama mafuta kutaendelea kupunguza gharama za uzalishaji na usafirishaji pamoja na kutoa ruzuku kwenye pembejeo za kilimo kutaongeza uzalishaji wa nafaka.

Kuhusu mfumuko wa bei wa nchi mwaka jana, Dk. Chuwa alisema hadi Desemba ulikuwa asilimia 4.8.

"Bado Tanzania inafanya vizuri kwa upande wa udhibiti wa bei za bidhaa na huduma za jamii," alisema.

Takwimu zinaonyesha kuwa nchini Uganda, mfumuko wa bei mwaka jana ulikuwa asilimia 7.2 na Kenya asilimia 7.7 wakati nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), ni kati ya asilimia tatu hadi 7.0.

Utabiri wa NBS unakuja siku moja baada ya Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru, kutaja maeneo manne yatakayoisaidia Tanzania kukabiliana na mfumuko wa bei na kuleta unafuu ili nchi isiathirike zaidi kiuchumi.

Aidha, alisema mfumuko wa bei utaendelea kushuhudiwa kwa kuwa mitambo na mafuta ni bidhaa zinazonunuliwa kwenye mataifa makubwa ambayo yameathiriwa na mfumuko wa bei.

Alisema serikali inafanya jitihada, ili kuhakikisha nchi haikumbwi na uhaba wa chakula.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha nne kutoka Tabora hadi Isaka, chenye urefu wa kilomita 165, mkoani Shinyanga jana. Ujenzi huo, utakaogharimu Sh. trilioni 2.6, unatarajiwa kukamilika Machi 2026. Kushoto ni Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa. **PICHA: MARCO MADUHU**

# 'Kichaka' uchakachuaji mbolea ruzuku chabainika

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KAMATI ya Ulinzi na Usalama, Mkoa wa Njombe imebaini nyumba chakavu katika Mtaa wa Ramadhani, mjini Njombe inayodaiwa kutumiwa na mfanyabiashara mmoja (jina limehifadhiwa), kuchakachua mbolea ya ruzuku.

Ndani ya nyumba hiyo ilikutwa shehena ya mifuko ya mbolea za ruzuku aina mbalimbali zikiwamo Urea, Can na OCP na mifuko mitupu, mashine moja ya kushonea pamoja na majenereta mawili.

Imedaiwa kuwa nyumba hiyo inatumika kufanya udanganyifu wa kuchanganya mbolea hizo kisha kuuzwa kwa wakulima.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika eneo hilo, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, alisema kamati hiyo ilibaini tukio hilo Januari 17, mwaka huu majira ya saa nne usiku baada ya kupata taarifa za siri.

"Tumebaini uwapo wa nyumba ambayo kuna mfanyabiashara anaitumia kuchakachua mbolea, kwa hiyo tumejionea wenyewe marobota ya mifuko yakiwa yametoka kiwandani kwa jina lake na tumekuta nyumba hii haina umeme na jenereta mbili," alisema Mtaka.

"Nimeelekeza maduka yote ya mfanyabiashara huyu yawekwe chini ya ulinzi na upekuzi ufanyike nyumbani kwake ili tujiridhishe kama bidhaa hii ni kwa kiasi gani inafanana na ya dukani kwake na tumeelekeza mamlaka inayosimamia mbolea kusimamisha leseni ya mfanyabiashara huyu," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamis Issah, amehakikishia kamati ya ulinzi na usalama pamoja na wananchi wa mkoa huo kuwa wanakwenda kuweka nguvu, ili kuhakikisha jambo hilo linashughulikiwa na kukomeshwa.

Diwani wa Kata ya Ramandhani, Nickson Nganyange, alisema waligundua uchakachuaji mkubwa wa mbolea uliokuwa unafanyika kwa siri.

"Huu mchanganyiko unaofanyika wananchi hawajui wanaweka minjingu kuipeleka DAP kukuzia halafu wananchi hawajui mwisho wa siku matokeo hakuna," alisema Nganyange.

Awali, Mwenyekiti wa Mtaa wa Ramadhani, Evaristo Mwimba, alisema walipokea taarifa kutoka kwa wananchi ya uwapo watu ambao hawafahamiki wakiwa wanashusha vifaa kutoka kwenye guta.

"Baada ya kupokea taarifa hiyo nilifika eneo la tukio nikakuta mlango mmoja wa upande wa kushoto haujafungwa kuna mifuko mitupu ya mbolea na mlango mwingine umefungwa na kufuli tukaangalia pembeni kwenye uwazi kulikuwa na mbolea ziko ndani," alisema na kuongeza:

"Tulipiga simu polisi walikuja askari hapa eneo la tukio wakavunja mlango wakakuta mifuko mingine imeandikwa ruzuku na mingine haijaandikwa, baada ya hapo wananchi walileta taharuki kwa kulalamika baadhi ya mbolea ujazo wake sio sahihi lakini hatukua na vielelezo rahisi vya kulisemea."

Mwimba alisema wananchi wa Njombe wanategemea kilimo na kunapotokea ujanja wa namna hiyo unaweza kusababisha kushusha uchumi.

Mkazi wa Mtaa wa Ramadhani, Makrina Mgaya, alisema jambo hilo limewaumiza kwa sababu maisha yao yanategemea kilimo.

"Tunasomesha watoto kupitia kilimo, anafeli kupeleka mahindi shuleni kwa sababu ya kukosa mahindi, tunaomba serikali imchukulie hatua kali kwa sababu mtu huyu ni muuaji ameua wananchi wangapi, mtu amechukua mbolea mifuko 25 yote feki," alisema Mgaya.

# Afa kwa kuangukiwa na mti akimwokoa mwanawe

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kijiji cha Makonjiganga, Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Fadhira Mtou (36), amefariki dunia papo hapo baada ya kudondokewa na mti mkubwa aina ya Msufi wakati akimwokoa mtoto wake aliyekuwa ndani ya nyumba yao akiwa amelala.

Taarifa kutoka katika kijiji hicho zilizothibitishwa na viongozi mbalimbali, akiwamo Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho Mariamu Malua, zimeeleza kuwa Fadhira alikutwa na umauti huo juzi saa 8:30 mchana.

Mwenyekiti Malua alisema siku hiyo Fadhira akiwa nyumba ya jirani, mvua kubwa iliyoambatana na upepo mkali ilinyesha na kusababisha madhara, ikiwamo kuangusha mazao, minazi, mipapai, mikorosho na miembe.

Alisema Fadhira akiwa amesimama katika nyumba hiyo kujificha na mvua iliyokuwa ikiendelea kunyesha, alikumbuka ndani ya nyumba yake kuna mtoto aliyetajwa kwa jina la Yaluva aliyekuwa amelala na kuamua kujitosa kwenda kumwokoa dhidi ya miti iliyokuwa ikiangushwa na upepo isiathiri nyumba yao.

"Huyu mama baada ya kuona upepo ukidondosha mazao yakiwamo minazi, mikorosho, minazi na miembe, alikwenda ndani ya nyumba yao kumwokoa mtoto wake," alisema Malua.

Mwenyekiti huyo alisema baada ya kutoka nae nje ya nyumba kwenda nyumba ya jirani, mti mkubwa aina ya msufi ulianguka na kumkandamiza mama na kufariki dunia papo hapo, huku mtoto akijeruhiwa mguu wake wa kulia.

Alisema kutokana na kifo hicho, wananchi waliokuwapo eneo la tukio walimchukuwa mtoto na kumpeleka Hospitali ya Wilaya ya Liwale kwa matibabu, wakati mwili wa mama yake ukichukuliwa na kaka yake, Adamu Mtou, kuupeleka nyumbani kwake kuendelea na taratibu za mazishi.

Kaka wa marehemu, Mtou, alikiri dada yake kufariki dunia kwa kuangukiwa na mti alipokuwa akienda kujificha mvua nyumba ya jirani yake na kwamba mpwa wake, Yalua, amevunjika mguu wa kulia na amefungwa bandeji ngumu (POP) na sasa anaishi naye nyumbani kwake.

Mkuu wa Wilaya ya Liwale, Judithi Nguli, amekiri kutokea kwa tukio hilo na pamoja mtoto huyo kujeruhiwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP) Pili Mande, amekiri kutokea kwa tukio hilo ambalo limesababisha kifo cha mwanamke huyo aliyekuwa akijaribu kumwokoa mtoto wake.

# Mpango awa mbogo uhujumu reli ya SGR

**Na Frank Monyo,** SHINYANGA

MAKAMU wa Rais, Dk. Phillip Mpango, ameviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuwasaka na kuwakamata baadhi ya askari polisi wanaoshirikiana na wananchi katika wizi wa miundombinu ya miradi ya kimkakati ikiwamo reli ya kisasa (SGR).

Dk. Mpango alitoa agizo hilo jana katika Kijiji cha Isaka Stesheni mkoani Shinyanga wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa kipande cha nne cha SGR kutoka Tabora hadi Isaka chenye urefu wa kilomita 165.

Alisema anazo taarifa za wizi wa vifaa vya ujenzi hasa mafuta, nondo na saruji na baadhi ya watu wanaofanya uharifu huo ni wafanyakazi wasio waaminifu walioajiriwa na makandarasi na baadhi ya askari polisi.

"Wako madereva wa magari (katika miradi), wamo waendeshaji wa mitambo na hata baadhi ya wakazi wa maeneo jirani na mradi wanashiriki katika wizi wa miundombinu ya miradi jambo ambalo ni kuhujumu uchumi na watu hao hawaitakii mema nchi yetu," alisema.

"Naviagiza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama viwasake wahusika wote wawakamate na wawachukulie hatua. Na kwa upande wa wale watu wanaonunua mali za wizi kutoka katika miradi hii ya ujenzi wa reli yetu, pia wakamatwe. Wako watu wanaonunua mafuta wanapeleka mgodini, kwa hiyo naviagiza vyombo vya ulinzi na usalama vibaini mtandao mzima nao wakamatwe na wachukuliwe hatua za kisheria," alisisitiza Dk. Mpango

Alisema Rais Samia suluhu Hassan 'anavuja jasho la damu' akitafuta fedha za kuendesha miradi mbalimbali nchini halafu watu wachache wanahujumu na kueleza kuwa serikali haitawavumilia watu hao.

"Ninazo taarifa kuwa wako baadhi ya askari wachache ambao nao wanajihusisha na huo wizi, si tu kwamba naagiza wakome lakini nao wasakwe na wakamatwe, washughulikiwe kwa mujibu wa sheria zikiwamo sheria za kijeshi.

"Askari wa Tanzania ni askari wenye nidhamu. Hatuwezi kuwa na askari polisi ambao nao wanashiriki na kuwezesha wizi na kuhujumu miundombinu ya taifa letu na kamwe hatuwezi kuwachekea," alisema Dk. Mpango.

Alisema pamoja na ujenzi wa reli hiyo, tayari serikali imeingia mkataba wa kununua mabehewa 89, vichwa vya treni ya umeme 19 na seti za treni ya kisasa 10 na vyote vinagharama ya Shilingi trilioni 1.2.

"Waziri (wa Ujenzi, Prof. Makame Mbarawa) napenda kusisitiza wizara yako na shirika la reli kufatilia kwa karibu mchakato mzima wa kupata hivyo vifaa na kukamilike kwa wakati ili kuwezesha reli yetu ya kisasa kuanza kutoa huduma mara ujenzi wa miundombinu utakapokamilika," alisema.

MAKALA MAALUM

# Spika Bunge la India ataja mambo muhimu ya ushirikiano na Tanzania

Na Mwandishi Wetu

WAJUMBE wa Bunge la India wamekuja nchini Tanzania ikiwa ni ziara ya kuimarisha uhusiano baina ya nchi hizo mbili. Spika wa Bunge hilo, Om Birla (pichani), anaeleza kwa kina umuhimu wake katika mahojiano maalumu.



**SWALI:** Unaweza kutueleza kuhusu ajenda ya ziara yako nchini Tanzania na Watanzania watarajie nini?

**JIBU:** Tunaamini kwamba ziara ya sasa ya Wajumbe wa Bunge la India Tanzania ni muhimu katika historia ya kuimarisha uhusiano kati ya nchi hizi mbili ambao umeimarika katika miaka ya hivi karibuni, na kuwa ushirikiano wa kisasa na wa kiutendaji kwa kutilia mkazo zaidi biashara, uwekezaji na uchumi. Maingiliano, ushirika wa kimaendeleo unaojumuisha kujenga uwezo, mafunzo, mikopo yenye masharti nafuu na ruzuku na maelewano katika ngazi ya kisiasa.

Uhusiano wa India na Tanzania unatambulika kwa urafiki na ukaribu wa muda mrefu, mahusiano mazuri ya kiuchumi, ushirikiano mpana na wa kimaendeleo imara na uhusiano wa kihistoria wa ngazi ya watu wa nchi mbili hizi uliojengwa kwa mabadilishano ya kibiashara ya karne nyingi.

Ziara za mara kwa mara za ngazi ya juu kati ya nchi zetu zimekuwa kipengele muhimu cha uhusiano mzuri wa kisiasa, maelewano na kuthaminiana kwa miaka hamsini iliyopita. Ziara yetu ya sasa ina umuhimu wa pekee ambayo inakuja miaka hamsini baada ya ziara ya ujumbe wa Bunge la India uliooongozwa na Dk. G.S. Dhillon, Spika wa Bunge la India (Lok Sabha) tarehe 10 - 13 Oktoba, 1972.

India inaamini katika falsafa ya Vasudhaiva Kutumbakam (Dunia ni kama familia moja). Kwa vile taasisi za Bunge ni nguzo kuu za utawala wa kidemokrasia; itakuwa vyema kwa mataifa yetu yote mawili kuhimiza maingiliano ya mara kwa mara baina ya mabunge yetu na wabunge. Nina hakika ziara hii itaimarisha zaidi na zaidi uhusiano wetu wa nchi hizi mbili.

**SWALI:** Bunge la India linashirikiana vipi na serikali kuharakisha mfumo wa kisheria unaohitajika kurekebisha sekta muhimu za kiuchumi kama vile kilimo, elimu na nyinginezo?

**JIBU:** Bunge la India kama taasisi kuu ya kidemokrasia nchini, daima limekuwa mstari wa mbele katika kutafsiri maadili ya kikatiba kwa vitendo kwa kutunga sheria zinazofaa kujenga mustakabali bora wa jamii. Kwa mamlaka kutoka katika Katiba na maagizo yaliyotolewa katika kanuni kuu za sera ya nchi, Bunge la India limekuwa likitunga sheria zinazofaa kwa miaka ili kuendana na wakati na mahitaji.

Kwa kutunga sheria kadhaa za kimaendeleo, Bunge letu limetoa mwelekeo na kusaidia watu kutimiza ndoto zao - kijamii, kielimu na kiuchumi. Kuna sheria nyingi za kihistoria zilizotungwa na Bunge letu zikiwamo: Sheria ya Makampuni, 1956; Sheria ya Mishahara Sawa, 1976; Sheria ya Marufuku na Udhibiti wa Ajira kwa Watoto, 1986; Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa, 2005; Sheria ya Kitaifa ya Dhamana ya Ajira Vijijini ya Mahatma Gandhi, 2005; Sheria ya Haki ya Mtoto ya Kupata Elimu Bila Malipo na ya Lazima, ya mwaka 2009; Sheria ya Taifa ya Hifadhi ya Chakula, 2013; Sheria Kuu ya GST, 2017; na The Integrated GST Act, 2017; miongoni mwa nyingine.

Sheria hizi zote ni muhimu kwa mabadiliko ya kijamii na Bunge limeongoza kwa mfano na kuonyesha ukomavu na busara zake kwa miaka mingi kwa kuleta maelewano juu ya sheria mbalimbali muhimu. Vyama vyetu vya siasa pia vimechukua nafasi kubwa katika suala hili kwa kuweka kando tofauti zao za kisiasa na kushikana mikono pamoja linapokuja suala la sheria muhimu zinazohusu masuala ya kitaifa.

**SWALI:** Chini ya uongozi wako, ni mafanikio gani makubwa na hatua muhimu kwa Bunge la India? Je, kuna uzoefu/mafanikio yoyote kama haya ambayo Tanzania inaweza kujifunza kutoka India?

**JIBU:** Imekaribia miaka minne sasa ambapo nimekuwa na fursa ya kuongoza Bunge la India (Lok Sabha) ambalo ni Bunge lenye demokrasia kubwa zaidi duniani. Nimefurahishwa na ushirikiano na uungwaji mkono usio na kifani wa waheshimiwa wabunge ambao umekuwa chanzo cha msukumo wa mara kwa mara kwangu.

Ni Bunge la 17 (Lok Sabha), katika safari yake hadi sasa, limekuwa na mafanikio mengi ya kihistoria. Kulikuwa na sheria zinazofungua njia, majadiliano ya busara, mijadala yenye kujenga, mapendekezo ya kamati muhimu, mipango ya kufikia watu, miongoni mwa mengine, ambayo yote yalishikilia matarajio ya watu na ndoto ya India Mpya.

Imekuwa ni juhudi yetu ya mara kwa mara kuunda mazingira wezeshi kwa wanachama waheshimiwa, pamoja na vistawishi vyote muhimu vya kazi, usaidizi mahiri wa taarifa za utafiti, miundombinu ya hali ya juu, na zana za kisasa za teknolojia ya habari. Kando na hayo, vikao vya uhamasishaji kuhusu masuala ya mada, programu za kujenga uwezo, vituo vya ustawi, kambi za afya, rasilimali za kielektroniki zinazopatikana kwa urahisi, na msaada wa matibabu wa haraka, vilihakikishwa ili kuwezesha ushiriki wenye tija wa waheshimiwa wajumbe katika Bunge.

Bunge la India daima linahimiza uimarishaji wa mila za kidemokrasia na taasisi nchini India. Tukishiriki wazo la 'Taifa Moja, Jukwaa Moja la Kutunga Sheria' kama lilivyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Shri Narendra Modi, tunachukua hatua za kulitimiza kwa msingi wa kipaumbele. Kupitia mpango huu, shughuli za mabunge yote - mabunge yote mawili na Mabaraza ya Jimbo na Mabaraza ya Kutunga Sheria yatapatikana kwenye jukwaa moja.

Jengo jipya la Bunge ambalo liko ukingoni mwa kukamilika litakuwa pia muhimu katika historia ya Bunge la India na tukio muhimu katika kuadhimisha Aazadi ka Amrit Mahotsav, kuadhimisha miaka 75 tukufu ya Uhuru wetu. Jengo jipya limebuniwa na kujengwa ili kuwa na vifaa vya kisasa zaidi ili kukidhi mahitaji yote ya Bunge la kisasa na pia mahitaji yanayotarajiwa ya nyakati zijazo.

Bunge la Tanzania, kama vile wenzao, katika nchi nyingine ndilo Bunge Kuu la nchi. Sina shaka kwamba Bunge la Tanzania, kama India lingeendelea kubadilika kulingana na mahitaji ya mabadiliko ya nyakati.

**SWALI:** Tungependa kujua sheria mbalimbali za India kuhusu uwekezaji na jinsi Bunge kupitia sheria hizo zinavyokuza ustawi wa uchumi wa nchi.

**JIBU:** Leo hii, India ni mojawapo ya maeneo yanayopendelewa zaidi kwa uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni (FDI) kutokana na sera yake huria ya FDI, misingi imara ya uchumi mkuu, mfumo wake wa utawala wa kidemokrasia na uboreshaji wa nafasi yake katika Ripoti ya Benki ya Dunia ya Urahisi wa Kufanya Biashara. Jumla ya Uwekezaji wa Moja kwa Moja wa Kigeni nchini uliongezeka kutoka Dola 81,973 milioni katika Mwaka wa Fedha wa 2021 hadi Dola milioni 84,835 katika Mwaka wa Fedha wa 2022, jambo linaloakisi ongezeko la fursa za uwekezaji wa kigeni nchini. Ili kukuza uwekezaji, yamefanywa katika sekta kama vile Ulinzi, Bima, Petroli na Gesi Asilia na Mawasiliano (Simu). Zaidi katika sekta ya biashara, asilimia 100, FDI inaruhusiwa katika Biashara ya Rejareja ya Bidhaa Moja (SBRT) na asilimia 51, FDI inaruhusiwa katika Uuzaji wa Bidhaa Mbalimbali (MBRT).

Serikali imezindua mpango wa "Make in India" ili kuwezesha uwekezaji, kukuza uvumbuzi, kujenga miundombinu bora zaidi ya darasa na kuifanya India kuwa kitovu cha utengenezaji, uundaji na uvumbuzi. Shughuli za kufikia uwekezaji zinafanywa kupitia wizara, Serikali za Majimbo na Balozi za India nje ya nchi kwa ajili ya kuimarisha ushirikiano wa kimataifa na kukuza uwekezaji wa kigeni nchini.

Sheria muhimu zinazosimamia uwekezaji wa kigeni nchini India ni Sera ya FDI, iliyotolewa na DPIIT; na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Kigeni ya 1999 (FEMA), na sheria na kanuni zilizoundwa kuzihusu. Pia, Benki Kuu ya India (RBI) ilitoa Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Kigeni (Njia ya Malipo na Kuripoti Hati Zisizo za Madeni) za 2019, kwa uwekezaji nchini India na mtu anayeishi nje ya India.

Katika siku za hivi karibuni, Bunge la India limepitisha sheria nyingi zikiwamo: Sheria ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi, 2005; Sheria ya Maendeleo ya Biashara Ndogo Ndogo na za Kati, 2006; Sheria Kuu ya Ushuru wa Bidhaa na Huduma, 2017; Kanuni ya Ufilisi na kufilisika, 2021; Muswada wa Sheria (Marekebisho) wa Sheria za Bima, 2021; kuifanya India kuwa taifa la kuvutia na lenye urafiki kwa wawekezaji na kuchochea ukuaji. Nia ni kuondoa vikwazo vya kisera ambavyo vinaweza kuwa vinazuia uwekezaji kuingia nchini. Mabadiliko yanafanywa katika sera baada ya kuwa na mashauriano ya kina na washikadau ikiwa ni pamoja na vyama vikuu vya sekta, mashirika, wawakilishi wa viwanda/vikundi na mashirika mengine kwa kuzingatia maoni yao.

**SWALI:** India sasa ni nchi ya tano kwa uchumi mkubwa duniani. Ni mshirika muhimu wa kibiashara wa Tanzania. Je, inawezaje kuisaidia Tanzania katika kukuza mauzo ya nje na maendeleo ya viwanda?

**JIBU:** India inatoa asilimia 98 ya mpango wa bila ushuru kwa Tanzania. Hii imesaidia kukuza mauzo ya Tanzania kwenda India. Mwaka jana tulikuwa na uwiano wa biashara baina ya Dola za Kimarekani bilioni 4.58 na Dola bilioni 2.2 za mauzo ya nje kutoka Tanzania. India imesalia kuwa kivutio cha kwanza kwa Tanzania. Kwa mujibu wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), uwekezaji wetu tangu mwaka 1990 umefikia Dola za Kimarekani bilioni 3.68. Katika mwaka mmoja uliopita kumekuwa na mwelekeo mzuri wa uwekezaji katika usindikaji wa mazao ya kilimo, chanjo za wanyama, dawa, hospitali na bandari na mengine. India pia inafanya kazi na Tanzania katika kujenga uwezo kwa watu wake (capacity building).

HABARI KITAIFA

# Wakala 'abambwa' akidaiwa kuuza mbegu kwa bei ya juu

**Na Valentine Oforo,**
DODOMA

WAKALA wa Mbegu za Kilimo Tanzania (ASA) umesitisha mkataba wa wakala wa kuuza mbegu zake jijini Dodoma baada ya kubainika kuuza mbegu za ruzuku za alizeti kinyume cha bei elekezi iliyowekwa na serikali.

Pamoja na kusitisha mkataba huo, Jeshi la Polisi Dodoma linamshikilia wakala huyo, Wema Seth, kwa ajili ya kumhoji kabla ya kuchukua hatua zaidi za kisheria kwa tuhuza za kuhujumu jitihada za serikali za kuinua sekta ya kilimo.

Meneja wa Masoko wa ASA, Edward Mbugi, alisema uamuzi huo ulifikiwa jana baada ya kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika duka la wakala huyo jijini hapo.

Alisema kwenye ukaguzi huo, walibaini wakala huyo akiuza mbegu za alizeti za aina ya rekodi kwa bei ya juu kinyume cha bei iliyowekwa na serikali.

"ASA ilizigawa mbegu hizo kwa mawakala wake katika maeneo mbalimbali nchini kwa gharama ya Sh. 4,500 kwa kilo moja na kuwaagiza mawakala hao kuwauzia wakulima kwa Sh. 5,000 kwa kila kilo. Lakini Wema Agrovet amebainika kuuza mbegu hizo kwa Sh. 15,000 kwa mfuko wa kilo 2, badala ya Sh. 10,000," alisema. Mbugi aliwataka mawakala wote za ASA nchini kuzingatia sheria na maagizo yaliyotolewa na serikali katika uuzaji wa mbegu za ruzuku.

"Jambo hili alilolifanya Wemma linasikitishia sana kwani kabla ya kuingia mkataba tulimwalika na akahudhuria mafunzo maalumu ya namna ya kuuza mbegu hizi. Sasa sijui kwa nini amejiingiza katika uvunjaji huu wa sheria husika," alisema.

Mratibu wa Utoaji wa Mbegu za Alizeti kutoka ASA, Benjamin Mfupe, alisisitiza kuwa ASA haitamvumilia wakala wake yeyote ambaye atabainika kutoa huduma kwa wakulima kinyume cha sheria zilizowekwa, ikiwa ni pamoja na kupandisha bei ya mbegu za ruzuku.

"Huu ni mwanzo tu kwani kwa sasa tunajipanga kuanza msako mkali nchi nzima ili kukagua na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya mawakala wote wanaodhoofisha juhudi zinazofanywa na serikali kuwasaidia wakulima lakini pia kukuza zao la alizeti nchini," alionya.



Mbunge wa Kilosa, Prof. Palamagamba Kabudi (kushoto), akijadiliana jambo na Mbunge wa Ismani, William Lukuvi, walipokutana katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Washtakiwa waachiwa huru kesi ya mauaji

**Na Kulwa Mzee**

WAKAZI wa jijini Dar es Salaam, Masoud Iddi maarufu Maudomo na Abuu Vunja, waliokuwa wakikabiliwa na kesi ya mauaji ya Issa Juma, wameachiwa huru baada ya upande wa Jamhuri kushindwa kuthibitisha kosa lao.

Washtakiwa hao waliachiwa huru jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Ramadhani Rugemalila, aliyepewa mamlaka ya nyongeza kusikiliza kesi hiyo.

Washtakiwa waliachiwa huru baada ya mahakama kuona upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha kosa hilo bila kuacha shaka.

"Mahakama inaona upande wa mashtaka uliegemea ushahidi wa Baraka Hamisi ambaye katika maelezo yake anadai kushuhudia washtakiwa hao wakishirikiana na mtu mwingine aliyetajwa kwa jina la Mbaraka au Muba kumshambulia mtu asiyemjua.

"Hamisi alieleza aliona wazi tukio hilo lililotokea saa 2:00 usiku na kulikuwa na mwanga wa taa za umeme, washtakiwa hao na Muba walimpiga mtu huyo kisu cha shingoni, mgongoni na chini ya kifua. Kikanuni ushahidi wa utambuzi wa macho lazima mahakama uupitie, ijiridhishe kama hauna makosa ya kiutambuzi.

"Katika kesi hii, kuna mgongano wa ushahidi wa mashahidi wa upande wa mashtaka kwani wakati Hamisi akisema eneo la tukio kulikuwa na mwanga wa kutosha, mashahidi wenzake akiwamo askari mpelelezi alisema kulikuwa na giza," alisema Hakimu.

Alisema askari alidai kulikuwa na giza na wananchi walitumia tochi za simu zao kutambua mwili, hivyo kama kungekuwa na mwanga, askari asingesema kulikuwa hakuna mwanga na wananchi kutumia tochi za simu kutambua mwili wa marehemu.

"Kutokana na hali hiyo, ushahidi wa Hamisi mahakama haiwezi kuutumia kuwatia hatiani washtakiwa katika kesi kubwa kama hii kwa sababu kuna uwezekano washtakiwa hawakutambuliwa," alisema.

Hakimu alisema kwa kuwa hakuna ushahidi mwingine wa kuwatia hatiani washtakiwa, upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha kosa hilo na mahakama inawaachia huru.

Katika kesi hiyo washtakiwa hao walidaiwa kutenda kosa hilo Agosti 15, 2017 eneo la Tandika, Kilimahewa wilayani Temeke, Dar es Salaam.

# Waziri ataka uwekezaji teknolojia ya kidigitali

**Na Christina Mwakangale**

NAIBU Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, amewaagiza wadau wa sekta za fedha na bima, kujikita kwenye teknolojia ya kidigitali ili kuwa na uwekezaji kwenye uchumi endelevu.

Kigahe aliyasema hayo jana kwenye mkutano wa kujadili uchumi wa kidigitali kuelekea miaka 50 tangu kuanzishwa kwa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), jijini Dar es Salaam.

Katika mkutano huo, mada mbalimbali ziliwasilisha na uliwakutanisha wadau wa taasisi za fedha, bima, vyuo vya fedha wakiwamo wawakilishi kutoka serikalini na wanafunzi kutoka vyuo mbalimbali.

Akifungua mkutano huo kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema serikali imebaini kuwa changamoto iliyoko sasa si katika kuvutia wawekezaji pekee, bali ni namna ya kuwa na uwekezaji endelevu.

"Kumbukumbu ya miaka 50 tangu chuo kianzishwe iendane na kaulimbiu ya uchumi wa kidigitali, kwamba wataalamu wa fedha, bima na wadau wengine waone haja ya kuingia katika kizazi cha dunia ya kidigitali.

"Wizara itahamasisha uwekezaji katika sekta zote na uchumi jumuishi hasa kwenye viwanda. Changamoto kubwa si kuvutia uwekezaji bali namna ya kufanya uwe endelevu. Miaka iliyopita wawekezaji waliona uwekezaji haukui vizuri," alisema naibu waziri huyo.

Mkuu wa IFM, Prof. Joseph Lotta, alisema katika chuo hicho zimeanzishwa kozi mpya kuendana na kujua matumizi ya kidigitali, ambazo zinatoa mafunzo ili kudhibiti uhalifu mtandaoni katika sekta za bima na fedha.

Alisema mwaka ujao wa masomo, mitaala imeboreshwa na miaka ikianzishwa, ikiwa na lengo la kuwapa ujuzi wataalamu ndani ya sekta hizo, kukabiliana na wizi ama uhalifu mtandaoni.

"Tuko katika kizazi cha digitali ipo haja ya kuendana na mabadiliko haya, utaweza kunufaisha maendeleo ya kiuchumi. Mkutano huu umehusisha wadau kadhaa na mada tofauti zitajadiliwa siku mbili," alisema Lotta.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu wa Chuo cha Bima na Hifadhi ya Jamii Afrika Mashariki (ACISP), Sosthenes Kewe, alisema teknolojia ya kidigitali ni muhimu kwa ajili ya kudhibiti, kulinda, kukuza sekta hiyo, ambayo kwa kiwango kikubwa inawagusa watumiaji wengi kwa siku.

"Digitali inasaidia kuongeza uzalishaji, ajira, mapato na kuongeza thamani ya bidhaa ikiwamo zilizoko kwenye sekta ya kilimo ikiwamo mazao," alisema Kewe.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wananchi itikieni wito, pindi mnapoitwa kwenye mashauri

**JUZI** Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki Temeke, kilitoa takwimu kuonesha kwamba wanawake wanaongoza kwa kufungua mashauri ya ndoa, talaka na mirathi.

Kituo hicho kimeshahudumia mashauri 100,484 tangu kianzishwe, Oktoba mwaka jana.

Imeelezwa kuwa mashauri 55,773 ambayo ni sawa na asilimia 54 yalifunguliwa na wanawake, hali inayoonesha kuwa wengi wao wanajua umuhimu wa kudai haki zao kupitia njia sahihi za utoaji haki hasa linapotokea suala la ndugu kugombea mirathi.

Jaji Mfawidhi wa Mahakamu Kuu Kanda ya Temeke, Ilvin Mgeta, anafafanua kuwa idadi hiyo kubwa ya wanawake inatokana na wengi wao kupitia wakati mgumu wanapofiwa na waume zao kwenye masuala ya mali tofauti na wanaume wanapofiwa na wake zao.

Hali ya kugombea mali mwanamke anapofiwa na mume, hasa kutoka kwa ndugu wa mume ndiyo sababu mashauri ya wanawake kuwa mengi, kwa mujibu wa Jaji Mgeta.

"Kwa kuona hali hiyo ndiyo maana tunaweka mazingira mazuri kumsaidia huyu mwanamke aliyeumizwa na huu mchakato anaopitia baada ya kufariki kwa mume wake asikilizwe bila upendeleo, lakini aridhike kwamba ametendewa haki."

Kwa mujibu wa Naibu Msajili wa Mahakama Kuu Kanda ya Temeke, Mary Moyo, mpaka wiki hii Ofisi ya Ustawi wa Jamii wa kituo hicho, imehudumia watu 1,329 wakiwamo wanawake 901 sawa na asilimia 68 na wanaume ni 428 ambayo ni sawa na asilimia 42.

Hata hivyo, hoja kwamba wanawake wanaonekana kupendelewa kwenye kituo hicho, ilielezwa kuwa haina ukweli kwa kuwa wengine wao ndiyo wanaofika kufungua mashauri kutokana na kupata matatizo wanapotelekezwa na watoto.

Huduma zinazotolewa na wadau mbalimbali wa Ustawi wa Jamii zinaonyesha kwamba idadi ya wanawake ni kubwa kulinganisha na wanaume kutokana na mazingira wanayopitia.

Inasemekana kuwa wanaume wengi hawajitokezi kudai haki zao kwa kuogopa fedheha au kuchekwa, hali inayosababisha waendelee kuumia na wengine kupoteza maisha kwa sababu ya msongo wa mawazo.

Kituo hicho kimeshatoa huduma kwa watu 2,811 na kati yao wanawake ni 1,878 sawa na asilimia 66 na 933 ni wanaume ambao ni sawa na asilimia 34.


"Sisi hatumpendelei mwanamke kwenye utoaji wa haki isipokuwa tunaweka mazingira wezeshi ili hata lile kundi linaloonekana kuwa nyuma liwe katika mazingira sawa kwenye mchakato wa kupata haki na kwenye masuala haya mwanamke ndiye mwathirika zaidi ya mwanaume."

Katika hili, hakuna budi wananchi hasa wanaume kuhudhuria mahakamani kila wanapoitwa ili iwe rahisi kutenda haki kutokana na uzoefu kuonesha baadhi ya watu wamekuwa wakipuuzia wito wa mahakama na mwisho haki inapotolewa upande uliokuwa ukihudhuria kunakuwapo malalamiko kwamba haki haikutendeka na upendeleo.

Wahenga walisema usikatae wito kataa neno. Wananchi wanapoitwa kwenye mashauri ni lazima wawe wanatii wito kwa kufika mahakamani kwa wakati ili haki itolewe kwa wakati mfupi na wahusika waendelee kwenye shughuli zao za uzalishaji mali badala ya kila siku kushinda mahakamani kusikiliza mashauri.

Kunapokuwapo na pande zote mbili kwenye mashauri ni rahisi kupata suluhisho na haki kutolewa bila kuwapo malalamiko kuwa kuna upendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



## Wazazi, walimu pamoja tushirikiane kumlinda mtoto atimize ndoto zake

Na Halfani Chusi

**ILI** kukomesha utoro kwa wanafunzi na ukatili kwa watoto, wazazi wanapaswa kuweka kipaumbele kwenye kuchunguza na kufuatilia mienendo yao pindi wanapokuwa shuleni na nyumbani, ili kudhibiti vitendo hivyo.

Inasikitisha sana unapomwona mtoto ameshindwa kumaliza shule au kufaulu vizuri masomo yake, kwa kutohudhuria vizuri vipindi darasani, jambo linalodidimiza ukuaji wa elimu nchini.

Katika kupambana na ghasia hiyo wazazi wanapaswa kufuatilia mienendo ya watoto wao kuanzia shuleni mpaka nyumbani, kwa kukagua madaftari na ikibidi kuwasiliana na uongozi wa shule.

Wazazi wengi hawafuatilii mienendo ya watoto wao, wanapokuwa shuleni, jambo ambalo linalalamikiwa na walimu kwenye shule nyingi za msingi na sekondari kwamba hawatimizi majukumu yao ipasavyo.

Ni ukweli usiopingika kwamba, haiwezekani kukomesha tatizo la utoro pasina ushirikiano wa dhati kati ya mzazi, mwalimu na mtoto, mwalimu asipomwona mwanafunzi shuleni, anatakiwa kumuuliza mzazi na mzazi akimuona mtoto nyumbani anatakiwa amuulize kwa nini hajaenda shule.

Lakini, si utoro pekee ambao wazazi wanatakiwa kushirikiana na walimu bali hata masuala ya ukatili kwa watoto ikiwamo rushwa ya ngono ambayo ndio adui mkubwa wa maendeleo na ustawi wa jamii.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza, anatamka "Kama ushirikiano baina ya mzazi na mtoto au mzazi na mwalimu utakuwa hafifu haitokuwa rahisi kugundua, iwapo mtoto amekutana na vishawishi vya ukatili. "Mzazi anatakiwa mtoto wake anaporudi shuleni amuulize jinsi alivyoishi shuleni kwa siku hiyo na kumdadisi kama kuna mtu alimshika kwenye sehemu nyeti za mwili wake, mzazi hatakiwi kuwa mkali kwa mtoto wake kitendo hicho kitamfanya aogope kumwambia jambo la siri," anasema Janeth na kuongeza;

> **"Mzazi anatakiwa mtoto wake anaporudi shuleni amuulize jinsi alivyoishi shuleni kwa siku hiyo na kumdadisi kama kuna mtu alimshika kwenye sehemu nyeti za mwili wake, mzazi hatakiwi kuwa mkali kwa mtoto wake kitendo hicho kitamfanya aogope kumwambia jambo la siri,"**

"Mzazi anapaswa kumjengea mtoto mazingira ya kumwambia chochote hii itasaidia kufahamu mapema iwapo mtoto atafanyiwa kitendo kibaya."

Pamoja na yote, serikali inapaswa kuweka mkazo wa agizo lake kila gari la shule linatakiwa liwe na mwangalizi wa wanafunzi wa kike, jambo litakalosaidia kupunguza zile kesi zilizokuwa zinasikika kondakta wa gari la wanafunzi amewanajisi wanafunzi kadhaa.

Ni mtazamo chanya kwamba, mtoto anatakiwa kulindwa toka anavyotoka nyumbani hadi anavyofika shuleni na wakati wa kurudi pia, ikiwezekana mzazi ampeleke mwenyewe mtoto shuleni na ahakikishe amepokewa na mtu sahihi.

Kwa kifupi, matukio ya watoto kukatisha masomo na kufanyiwa vitendo vya ukatili hayatoisha, kama sehemu hizo hazitoungana na kuwa kitu kimoja.

Mtu ukifuatilia kwa kina pindi linapotokea suala ala ukatili wa kijinsia utagundua katika hao watu watatu, kuna mmoja hakutimiza jukumu lake ipasavyo.

Watoto ni taifa la kesho wanahitaji ulinzi ili watimize ndoto zao na sisi ndio watu wa kuwalinda kumlinda mtoto ni jukumu letu sote sio suala la mzazi na mwalimu pekee, unapomwona mtoto wa mwenzako anafanya kosa, inapaswa kumwonya na kumfundisha kitu sahihi cha kufanya. Huwa ni wajibu wa msingi kwa kila mzazi.

• Simu: +255 787879707

# Baba afungwa miaka 30 kwa kumnajisi mwanawe

**Na Said Hamdani,**
LINDI

MAHAKAMA ya Mkoa wa Lindi, imemuhukumu Athumani Manduta (49) kifungo cha miaka 30 jela kwa kukutwa na hatia ya kumnajisi mtoto aliyemzaa mwenye umri wa miaka 14.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Conslota Singano, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Kabla ya hukumu, mshtakiwa alipewa nafasi ya kujitetea na kuiomba mahakama imsamehe ili aendelee kuhudumia watoto wake kwa kuwa akipewa adhabu kubwa kuna hatari ya kukosa huduma zake.

Hakimu Singano alimuuliza Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Heri Ngulunga, iwapo ana kumbukumbu za makosa ya zamani kwa mshtakiwa na kujibu hakuna, lakini aliiomba mahakama kumpa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia ya aina hiyo.

Aidha, alidai kitendo kilichofanywa na mshtakiwa, kumnajisi mtoto wake wa kumzaa ni ukatili mkubwa na haustahili kuvumiliwa.

Hakimu Singano alimhukumu mshtakiwa kifungo cha miaka 30 jela.

Ilidaiwa mahakamani na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, kuwa mshtakiwa alimfanyia ukatili mtoto wake kwa kumnajisi ambaye ni mwanafunzi wa darasa la nne.



Mafundi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wakilaza mabomba katika mtaa wa Buza, Kata ya Buza, wilayani Temeke juzi, ikiwa ni utekelezaji wa mradi wa maji Jet-Buza awamu ya tatu utakaonufaisha wakazi takribani 173,810. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mama na mwana wahukumiwa kifungo miaka 20 jela

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, imewatia hatiani na kuwahukumu kifungo cha miaka 20 jela, Anna Uroki na mwanawe Dennis Uroki kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya.

Hukumu hiyo ilisomwa mbele ya Jaji Godfrey Isaya katika masijala ndogo ya Moshi baada ya pande zote mbili kufunga ushahidi.

"Upande wa Jamhuri umeweza kuthibitisha mashtaka dhidi ya mshtakiwa Dennis Uroki na Anna Uroki bila kuacha shaka, Mahakama inawatia hatiani na kumwachia huru mshtakiwa wa tatu, Mussa Temba kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya kinyume na sheria," alisema Jaji Isaya.

Washtakiwa katika kesi hiyo walishtakiwa kwa kosa la kusafirisha bangi kilo 351.

Inadaiwa walikamatwa Oktoba 17, 2020, maeneo ya Chillo Holili, wilayani Rombo, mkoani Kilimanjaro.

Upande wa Jamhuri katika usikilizwaji wa kesi uliwakilishwa na Wakili wa Serikali, Tully Helela na ulikuwa na mashahidi saba, washtakiwa walijitetea wenyewe kwa kuwakilishwa na Wakili Patrick Paul, Edina Solomon na Angel Mongi.

Jaji Isaya alisema katika kuwahukumu washtakiwa, mahakama imezingatia hoja za Wakili Tully kwamba biashara ya dawa za kulevya ina athari mbaya na inaathiri watu wa umri wote.

"Nachukulia pia washtakiwa ni wakosaji wa kwanza ambao wamekaa ndani, chini ya ulinzi kwa zaidi ya miaka miwili.

"Nikiwa na yote akilini mwangu, ninaongozwa na Sheria ya Udhibiti na Utekelezaji wa Dawa za Kulevya na Mwongozo wa hukumu wa Tanzania kwa maofisa wa Mahakama, ambayo inatoa kifungo cha chini cha miaka 20 hadi miaka 30 ambayo ni adhabu ya juu zaidi kwa mfungwa.

"Kwa kuwa watuhumiwa ni wahalifu ambao wamekaa Mahabusu Gerezani kwa zaidi ya miaka miwili, lakini tukikumbuka kuwa dawa za kulevya huleta hatari kubwa kwa jamii, afya na uchumi wa nchi ninawahukumu kila mmoja kwenda jela miaka 20," alisema Jaji Isaya.

Akisoma hukumu hiyo alisema mahakama inazingatia ushahidi wa shahidi wa kwanza unaoungwa mkono na kielelezo cha majani ambao unatosha kwamba majani yaliyomo kwenye mifuko saba ya salfa ilikuwa dawa za kulevya aina ya bangi kilo 351.01.

Alisema upande wa mashtaka ushahidi unaonyesha kuwa, Oktoba 17, 2020 saa tatu usiku, shahidi wa tatu na maofisa wengine wa polisi wakiwa katika doria katika eneo la Chilio, Holili alikamata gari lenye namba za usajili T175 AMX, Toyota Land Cruiser.

Alisema ndani ya gari walikuwa washtakiwa wawili (mshtakiwa wa kwanza na wa pili) pamoja na mifuko saba ya salfa ikiwa na majani makavu ambayo baadaye yalikuja kutambulika kuwa ni bangi.

Ushahidi wa Jamhuri ulidai mshtakiwa wa tatu aliibuka katika eneo la tukio alikuwa akiomba msaada wa washtakiwa waachiwe.

Jaji Isaya alisema washtakiwa wa kwanza na wapili katika sehemu ya utetezi wao walikana kuhusika katika tukio hilo, lakini walilalamika kwamba walilazimishwa kusaini hati ya ukamataji mali.

"Hili pia linachukuliwa kuwa wazo la baadaye kwani swali hilo lilikuwa halijaulizwa kwa shahidi wa tatu wakati anatoa ushahidi wala shahidi wa saba.

"Mshtakiwa wa tatu alikamatwa baada ya kutajwa na mshtakiwa wa kwanza na wa pili, katika kesi iliyoko hakuna kitendo chochote kilichoelezwa na upande wa mashtaka kufanywa na mshtakiwa wa tatu.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed






Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi (kulia) na Mkurugenzi wa Kampuni ya Computer Connections Limited, Umi Punja, wakitiliana saini nyaraka jijini Dar es Salaam jana, baada ya kampuni hiyo kukabidhi msaada wa kompyuta mpakato tano na mashine ya kuchujia maji vyenye thamani ya Sh. milioni 20 kwa ajili ya kuchangia kuboresha huduma katika hospitali hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake waongoza kufungua mashauri ya talaka, mirathi

**Na Joseph Mwendapole**

WANAWAKE wanaongoza kwa kufungua mashauri ya ndoa, talaka na mirathi kwenye Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki Temeke ambacho kimeshahudumia mashauri 100, 484 tangu kianzishwe Oktoba mwaka jana.

Kituo hicho kimejengwa maalum kwa ajili ya kushughulikia masuala ya ndoa, talaka na mirathi na kati ya yaliyofunguliwa, mashauri 55,773 sawa na asilimia 54 yalifunguliwa na wanawake na 44,711 sawa na asilimia 46 yalifunguliwa na wanaume.

Hayo yalisemwa jana na Jaji Mfawidhi wa Mahakamu Kuu Kanda ya Temeke, Ilvin Mgeta, wakati akizungumza kwenye kipindi cha Sema na Mahakama kinachorushwa na kituo cha ITV.

Alisema idadi hiyo kubwa ya wanawake inatokana na kupata wakati mgumu wanapofiwa na waume zao kwenye masuala ya mali tofauti na wanaume wanapofiwa na wake zao.

"Uzoefu unaonyesha wanawake wanapata wakati mgumu sana wa mirathi wanapofiwa na waume zao, lakini sio rahisi kukuta watu wanagombea mirathi anapokufa mwanamke na mwanamume kubaki ndiyo sababu mashauri ya wanawake yanakuwa mengi," alisema.

"Kwa kuona hali hiyo ndiyo maana tunaweka mazingira mazuri kumsaidia huyu mwanamke aliyeumizwa na huu mchakato anaopitia baada ya kufariki kwa mume wake asikilizwe bila upendeleo, lakini aridhike kwamba ametendewa haki na si kwamba wanapendelewa," alifafanua Jaji Mgeta.

Naye Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Kanda ya Temeke, Mary Moyo, alisema mpaka wiki hii Ofisi ya Ustawi wa Jamii wa kituo hicho, imehudumia watu 1,329 wakiwamo wanawake 901 sawa na asilimia 68 na wanaume ni 428 ambayo ni sawa na asilimia 42.

Akijibu madai kwamba wanawake wanaonekana kupendelewa kwenye kituo hicho, Mary alisema hakuna ukweli kwa kuwa wanawake wengi ndiyo wanaofika kufungua mashauri kutokana na kupata matatizo wanapotelekezwa na watoto.

Alisema hata huduma zinazotolewa na wadau mbalimbali wa ustawi wa jamii zinaonyesha kwamba idadi ya wanawake ni kubwa kulinganisha na wanaume kutokana na mazingira wanayopitia.

Mary alisema wadau hao wametoa huduma kwa watu 2,811 na kati yao wanawake ni 1,878 sawa na asilimia 66 na 933 ni wanaume ambao ni sawa na asilimia 34.

"Sisi hatumpendelei mwanamke kwenye utoaji wa haki isipokuwa tunaweka mazingira wezeshi ili hata lile kundi linaloonekana kuwa nyuma liwe katika mazingira sawa kwenye mchakato wa kupata haki na kwenye masuala haya mwanamke ndiye mwathirika zaidi ya mwanaume," alisema.

Aliwaomba wananchi kuhudhuria mahakamani kila wanapoitwa ili iwe rahisi kutenda haki kwa kuwa uzoefu unaonesha baadhi ya watu wanapuuzia wito wa mahakama, lakini mwisho wa siku wanalalamika haki haikutendeka.

"Kuna usemi wa Kiswahili kwamba usikatae wito kataa neno kwa hiyo wananchi wawe wanatii wanafika mahakamani kwa wakati ili haki itolewe kwa wakati mfupi na wahusika waendelee kwenye shughuli zao za uzalishaji mali badala ya kila siku kushinda mahakamani kusikiliza mashauri," alisema.

# Equity yazindua tumerahisisha kufikia wateja wengi kirahisi

**Na Roman Mallya**

BENKI ya Equity Tanzania imezindua kampeni yake ya mwaka 2023 'Tumerahisisha' yenye lengo la kusogeza zaidi huduma kwa wateja na bidhaa za kifedha kwa urahisi na kidijitali.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa kampeni hiyo jana, jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa benki hiyo, Isabella Maganga alisema, kwa kushirikiana pamoja wanakwenda kutimiza ndoto za wateja.

"Umoja wetu ndio utawezesha kufanikisha hili, Benki ya Equity tumerahisisha upatikanaji wa huduma zetu kwa njia za kimtandao, kupitia matawi tumeweka uhuru wa kupata huduma za kibenki," alisema.

Pia alisema benki yao imezifanya huduma kuwa za gharama nafuu zaidi na mteja azipate bila ya kuwa mzigo kwake.

"Tunataka machinga, mamalishe, mfanyakazi, mfanyabiashara mdogo, kati na mkubwa wote wawe wateja wetu. Tumeondoa mambo ya mchakato na urasimu kwa kufanya huduma zetu ziwe rahisi kwa kila anayeingia katika mtandao wetu aweze kujihudumia."

Kiongozi huyo alisema kwa wateja wanaoomba mkopo kupitia benki hiyo, wameondoa suala la mchakato au urasimu kwa kujali muda wao kwa kupata taarifa mapema hususan mtu anayetaka huduma ya kukopa.

"Matawi yetu yote wapo maofisa maalum wa kutoa ushauri wa kitaalamu wa kumsaidia mteja kutimiza malengo yake. Kwa upande wa huduma tumerahisisha kufungua akaunti ambapo mteja unaipata hapo hapo kwa kadi ya ATM, visa na kuunganishwa katika simu. Tumerahisisha huduma kupitia wakala kwa wateja wanaotaka kuweka au kutoa fedha na kulipa ankara mbalimbali," alisema.

Maganga alisema mwaka jana, Equity Group ilizindua Mpango wa Ufufuaji na Ustahimilivu wa Afrika, mpango wa mabadiliko ya kijamii na uchumi ambao Equity imejipatia mfuko wa Dola za Marekani bilioni saba.

Alisema imejipatia fedha hizo kwa lengo la kuathiri watu milioni 100 barani Afrika kupitia mipango yake ya athari za kifedha kwa kijamii na kufikia wajasiriamali milioni tano na wateja binafsi milioni 25, ili kutoa nafasi za ajira milioni 50.

# Balozi Concar ataka uandishi mahiri kuitangaza Afrika

**Na Restuta James**

BALOZI wa Uingereza nchini, David Concar, amewataka waandishi wa Afrika kuandika habari nzuri zinazoendelea barani humo kuanzia ubunifu, ukuaji wa uchumi na biashara.

Balozi Concar aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipokuwa akizindua tuzo ya umahiri wa uandishi ya Komla Dumor ambayo hutolewa na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC).

Alisema uandishi mahiri unahitajika Afrika kuieleza dunia mambo mazuri yaliyoko barani humo ikiwamo ukuaji wa uchumi, biashara, filamu, muziki, tamaduni na michezo mingine ikiwamo mpira wa miguu.

"Uandishi huu uonyeshe kwamba Afrika sio tu umaskini, vita na migogoro," alisema.

Aidha, alisema dunia inakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinahitaji uandishi wa habari mahiri utakaoibua mjadala na hoja ili kuzitatua.

Alisema pamoja na umuhimu mkubwa wa habari kwa sasa, uandishi mahiri unapotea kutokana na kusambaa haraka kwa taarifa za upotoshaji ambazo hazifanyiwi utafiti wa kina.

"Waandishi karibu kote duniani wanakabiliwa na changamoto ya malipo kidogo, kufanyakazi katika mazingira magumu au hatarishi na presha toka kwa makundi yenye maslahi maalumu kwenye baadhi ya habari," alisema.

Tuzo hiyo ambayo hutolewa kuibua na kukuza vipaji vipya vya uandishi barani Afrika, imekwenda kwa mwandishi wa Habari Dingindaba Buyoya wa Zambia.

Mshindi atapata fursa ya kuwa katika makao makuu ya BBC mjini London, kwa miezi mitatu kupata ujuzi na uzoefu.

BBC inawahimiza wanahabari kote barani Afrika kutuma maombi kwa ajili ya tuzo hiyo, ambayo inalenga kukuza na kusherehekea vipaji bora vya uandishi wa habari wanaoishi na kufanya kazi katika Bara la Afrika.

Akizungumza baada ya kupewa tuzo hiyo, Buyoya alisema: "Komla Dumor alinipa hamasa, hivyo kushinda tuzo na kushiriki katika urithi wake imekuwa heshima," Buyoya alisema.

"Ninawahimiza waandishi wa habari wa kiafrika kutuma maombi ya tuzo, ni njia ya kipekee ya kujifunza na kukuza zaidi ujuzi unaohitajika," alisema.





# Mapya yaibuka tozo ya utalii wa utamaduni Eyasi

**Na Woinde Shizza,**
KARATU

SIKU chache baada ya wakazi wa Tarafa ya Eyasi, Wilaya ya Karatu, mkoani Arusha, kulalamikia tozo ya Dola za Marekani 25 zinazotozwa na Halmashauri ya Wilaya hiyo kwa ajili ya shughuli za utalii wa kitamaduni, mapya yameibuka.

Hali hiyo imesababisha jamii ya warina asali, waokota matunda na mizizi ya Kihadzabe na wafugaji wa jamii ya Wadatoga, kutishia kuyahama makazi yao ili kuishinikiza Wizara ya Maliasili na Utalii, kuagiza kusitishwa kwa tozo hiyo. Kwa nyakati tofauti jana, wakiwa katika Kijiji cha Qand'end kilichoko Kata ya Baray, wilayani humo, viongozi wa jamii ya Wahadzabe, Ntontowasi Nuika na Kankono Thomas, walisema kutokana na tozo hiyo wameamua kusitisha shughuli za utalii wa kitamaduni ili kuonyesha kutokubaliana na tozo hiyo.

Kwa mujibu wa Nuika, jamii hiyo imekubaliana kuanzia sasa haitatoa ushirikiano kwa mtalii yoyote atakayeingia kutembelea jamii yao, huku wakimwomba Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, kwenda wilayani humo kutatua mgogoro huo kati yao na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu.

"Kiukweli hatupo tayari na hatutalipa hiyo tozo. Haiwezekani halmashauri imekuja na sheria mpya ya tozo za watalii inayokandamiza jamii, bila kuzingatia maslahi yetu. Jana, alikuja Mkuu wa Wilaya, kwenye kikao chake na sisi, lakini anaonekana kutubana ili tukubaliane na hiyo tozo, ambayo wao walioipitisha bila kutushirikisha. Sisi tumeogopa kwa sababu hatujazoea kuona bunduki,"alisema.

Aidha, Kankono Thomas, alisema halmashauri hiyo imepitisha kila mtalii anayeingia katika lango la Kijiji cha Qand'end, kufanya shughuli za utalii ikiwamo kuiona jamii ya Wahadzabe, Wadatoga na Wahunzi, kulipa Dola za Marekani 25 ambapo pesa hiyo ikigawanywa, jamii hizo zinaambulia Dola za Marekani mbili tofauti na hapo awali ambapo kila gari la utalii lilikuwa likilipa Dola za Marekani 110 na jamii hizo zikipata Dola za Marekani 20 kila moja.

Kutokana na mgogoro huo, jamii hizo zimemshutumu Mkuu wa Wilaya hiyo, Dady Kolimba, kwa kushindwa kuwasikiliza wawakilishi wao alipokutana nao pamoja na diwani wao, Elitumaini Rweyemamu.

Vilevile, Sabargwa Dandu kutoka jamii ya Wadatoka, alisema hawakubaliani na tozo hiyo ya utalii wa Lake Eyasi, akidai hawajashirikishwa, kwamba mabadiliko hayo na wao kama wadau wa utalii wameona hayana tija kwao.

Diwani wa Baray, Elitumaini Rweyemamu, akizungumzia mgogoro huo alisema kuwa hakuna kikao hata kimoja cha Baraza la Madiwani wilayani humo, kilichoketi na kupitisha agenda ya mabadiliko ya tozo za utalii katika lango la Qand'end.

Alipoulizwa kuhusu madai hayo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Daddy Kolimba, alisema kuwa makubaliano hayo yalipitishwa na baraza la madiwani na yeye kama mwakilishi wa serikali, analazimika kusimamia na kuhakikisha amani inakuwapo na kwamba hawezi kutengua uamuzi huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Karatu, Karia Magaro, alipoulizwa juu ya madai hayo, alisema tozo hiyo ilipitishwa baada ya makubaliano ya pande zote, kikiwamo Chama cha Waongoza Watalii nchini (TATO).




Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga, Rajabu Abdalla (katikati), akizungumza na baadhi ya viongozi wa chama hicho, baada ya kukabidhiwa rasmi ofisi yake juzi. Kushoto kwake ni Katibu wa CCM wa Mkoa huo, Suleiman Mzee Charasi. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Wanaume wapewa hadhari wenza wao kuwa na bodaboda maalum

**Na Oscar Assenga,** TANGA

KIONGOZI Mkuu wa Taasisi ya Kiislamu ya Almostafa Khai Riyyan ya jijini Tanga, Ahmad Janga, amesema kumeibuka tabia ya baadhi ya wanaume kuruhusu wenza wao kuwa na kijana maalumu wa kumbeba kwa pikipiki, kwamba hali hiyo ikiendelea bila kukemewa itavunja ndoa nyingi.

Janga, ambaye cheo chake kwa lugha ya Kiarabu anatambuliwa kama 'Mudir' aliyasema hayo jana alipokuwa Msikiti wa Barabara ya 17, kabla ya kufungisha ndoa 100 kwa wakati mmoja.

Katika nasaha zake alisema kuna athari kubwa kwa wanandoa kuwapa uhuru wake zao wa kuwa na waendesha pikipiki wao maarufu 'bodaboda' bila kuwa na wivu, jambo ambalo litachochea kuvunjika kwa ndoa nyingi kutokana na vijana hao kukosa uaminifu na kuwarubuni wanawake hao kuingia katika mahusiano mapya.

Alisema kwa kuwa vijana hao wanaotafuta riziki huyajua mambo mengi ya familia hizo wanazozibeba kwa pikipiki na wakati mwingine hulazimika kuwatunzia siri za ugomvi wana ndoa hao.

"Wengine unakuta ni wasichana wenye umri mdogo, hawa bodaboda huwaweka karibu na kuwachukulia kama ndugu zao na kuwafanya rafiki zao, kwa hiyo huwa rahisi kuwarubuni kuingia kwenye mahusiano na kinachofuata inapogundulika kuna mambo yamekwenda ndivyo sivyo, ndoa nyingi huvunjika na tunaona wanakuja kwetu kulalamika.

"Niwaambie kwamba hii Kiislamu halikubaliki, lazima tuwe na wivu na wake zetu na kuwahifadhi nyakati za sala.

Tunawaacha wake zetu wanaenda na bodaboda na wala hakuna kuona wivu, hii ni balaa. Ni makosa kuruhusu mambo haya machafu kufanyika,"alisema Mudir Janga.

Aidha, aliwasihi vijana hao waliongia kwenye ndoa, kuhifadhi nyumba zao na wawe na wivu na wenza wao na wasiache jukumu hilo kwa waendesha bodaboda, kwa kuwa jamii inakabiliwa na tatizo kubwa la mmomonyoko wa maadili.

Hata hivyo, aliwaonya waendesha pikipiki nchini, wasijigeuze wao ni maarufu kwa kuvunja ndoa za watu, kwa sababu ya kujua siri za wateja wao, badala yake wasaidie jamii kulinda mila na desturi.

# Asilimia 41.5 ya wanafunzi Arusha waripoti shuleni

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

OFISA Elimu Mkoa wa Arusha, Abel Ntupwa, amesema hadi sasa ni asilimia 41.5 ya wanafunzi waliojiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo 2023 wameripoti shuleni.

Wanafunzi hao ni kati ya 40,288 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika mkoa huo.

Akizungumzia jana jijini humo, Ntupwa, alisema kuwa mwitikio huo wa wanafunzi ni mkubwa kutokana ni wiki ya kwanza ya masomo toka shule za sekondari zifunguliwe na tayari masomo yameanza tangu Januari 9, mwaka 2023.

Kutokana na kiwango hicho kutoridhisha, aliagiza wazazi na walezi kuwawaisha wanafunzi shuleni ili waendelee na masomo bila kuchelewa.

Ntupwa alisema serikali ilitoa Sh. bilioni tano ili kuhakikisha vyumba vya madarasa vinajengwa katika shule za umma 268 za Mkoa wa Arusha.

"Matarajio yetu Mkoa wa Arusha katika shule za umma 268 ni kupokea wanafunzi 40,288 wa kidato cha kwanza kwa mwaka 2023 na hadi kufikia leo ni 41.5% wamesha jiunga katika halmashuri zetu zote saba za Mkoa wa Arusha," alisema na kuongeza:


"Niwasihi wazazi wote wahakikishe wanafunzi wote waliochaguliwa na kupangiwa shule wawapeleke mapema maana masomo yameshaanza na waache mila potofu ambazo hazina faida katika jamii zetu ambazo zinasababisha mtoto kukosa elimu," alisema.

Akifafanua juu ya uwiano wa wanafunzi walioanza masomo na viwango vinavyo takiwa katika kila Wilaya ya Mkoa wa Arusha ikiongozwa na Halmashauri ya Jiji la Arusha ni asilimia 58.7 ya wanafunzi walioripoti shule.

"Jumla ya wanafunzi ni 40,288 wanatakiwa kujinga na masomo ya kidato cha kwanza, ambapo Wilaya ya Karatu ni 4,952 walio jiunga ni 691 sawa na asilimia 14, Ngorongoro 3,089 waliojiunga ni 515 sawa na asilimia 16, Monduli 3,469 waliojiunga 941 sawa na asilimia 27.

Alisema: "Longido 1,693 waliojiunga 621 sawa na asilimia 37, Meru 7,017 waliojiunga ni 2,601 sawa na asilimia 37, Arusha DC 7, 945 waliojiunga 3,735 sawa na asilimia 47 na Arusha Jiji 12,423 waliojiunga ni 7,301 sawa na asilimia 58.7".

Aliongeza: "Katika hili kwanza niipongeze serikali kwa kuwapatia vijana wetu mitihani waliyokuwa wamefutiwa matokeo yao ili waweze kufanya upya na pili kongole kwa wanafunzi walituliza akili na wameweza kufaulu wote na sasa wanaenda kujiunga kidato cha kwanza na tayari serikali imesha wapangia shule."





# Wanafunzi 6,140 hawajaripoti kidato cha kwanza

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WANAFUNZI 6,140 kati ya 12,507 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza, hawajaripoti shuleni kwa ajili ya kuanza masomo.

Kati ya wanafunzi hao, 6,367 sawa na asilimia 53 pekee ndiyo wameripoti shuleni.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Massala, amepiga marufuku michango ya aina yoyote itakayosababisha wanafunzi wa kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo 2023 washindwe kuripoti shuleni.

Wanafunzi 12,507 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka huu walipaswa kuripoti shule walizopangiwa tangu zilipofunguliwa Januari 9, mwaka huu.

Massala alitoa agizo hilo juzi wakati wa ziara yake kwa shule za msingi na sekondari zilizoko Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela yenye lengo la kufuatilia mahudhurio ya kidato cha kwanza, awali na darasa la kwanza.

Aliwataka wakuu wa shule, maofisa elimu, viongozi wa mitaa na kata kuhakikisha watoto wote waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza wanaripoti shuleni na hakuna kuzuia mtoto yeyote kuingia darasani.

"Kuna wazazi mnawazuia eti sababu hawajajaza fomu za kujiunga na shule kwenye kile kipengele cha daktari, wengine kwa kukosa sare, wengine sijui hawana jembe, nasema marufuku kuzuia watoto kwa sababu ya michango yoyote," alisema Massala.

Aliagiza zichukuliwe hatua kwa wazazi watakaoshindwa kupeleka watoto wao shuleni pamoja na watendaji watakaokwamisha wanafunzi kuripoti shuleni.

Diwani wa Kata ya Mecco, Godlisten Kisanga, aliwataka viongozi wa mitaa kushirikiana ili kuhakikisha watoto wote wanaripoti shuleni.

Aliahidi kufuatilia mpango huo nyumba kwa nyumba ili kubaini watoto waliochaguliwa na hawajaripoti shuleni.

Mwakilishi wa Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Alex Mkusa, aliwapongeza walimu kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha halmashauri hiyo inaendelea kushika nafasi nzuri kitaifa huku akiwataka kuongeza juhudi katika ufundishaji.



Mtoto James Emmanuel wa Klabu ya Watafuta Njia (Pathfinder Club), kutoka Kanisa la Waadventista Wasabato Buzuruga jijini Mwanza, akishiriki mafunzo yaitwayo komando yenye lengo la kuwafanya vijana wadogo kuwa wakakamavu, yaliyofanyika Bariadi mkoani Simiyu hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi wenye ulemavu kusomeshwa bure

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga imepanga kusomeshwa bure wanafunzi 140 wenye ulemavu ili kuhakikisha wanatimiza ndoto zao kama walivyo wenzao wasiokuwa na tatizo hilo.

Wanafunzi hao watasomeshwa katika Shule ya Msingi Mwime iliyoko Kata ya Zongomela na kati ya hao sita watakuwa wenye ualbino, 35 wasiosikia, walemavu wa akili 29, viungo 39, wasioona 25, usonji mmoja, wasiozungumza watano na masomo yao yameanza mwaka huu.

Ofisa Elimu wa Wilaya ya Kahama, Makundi Maalumu, Agnes Ntalimbo, alisema hayo hivi karibuni wakati akizungumza na gazeti hili namna ambavyo wamekuwa wakiyasaidia makundi maalumu hususani wanafunzi ili kuhakikisha wanafunzi hao wanatimiza ndoto zao za kielimu.

Alisema katika manispaa hiyo kuna walemavu wengi, lakini wameanza kusomesha wanafunzi wenye ulemavu mkubwa katika Shule ya Msingi Mwime. "Tuna wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali 300 kati ya hao 140 wana ulemavu mkubwa, tumewachukua na kuwaweka katika shule ya msingi Mwime na kuwasomesha ikiwamo kuwapatia mahitaji yote muhimu ili watimize ndoto zao kama walivyo wengine," alisema Ntalimbo.

Kadhalika, alisema shule hiyo inahitaji walimu 30 wenye taaluma ya kuwafundisha wanafunzi hao, lakini kwa kuanzia wameanza na walimu wanane ambao walikuwa wakifundisha shule mbalimbali, wawili ni walimu wa kike na sita wa kiume.

Alisema kati ya walimu hao, watatu wana taaluma ya kufundisha wanafunzi wenye ulemavu wa akili, watatu kufundisha wasiosikia, mmoja anafundisha wasioona, mwingine mmoja ana uwezo wa kufundisha wanafunzi wenye ulemavu wa aina zote.

Ntalimbo alisema wanafunzi wenye ulemavu wa kawaida wataendelea kusoma katika shule zenye mchanganyiko wa wanafunzi wasiokuwa na ulemavu na wataendelea kubaini wengine ili wawasomeshe na watawashirikisha wenyeviti wa serikali za mitaa.

Mkazi wa Mtaa wa Mbulu katika Kata ya Nyasubi, Wilisoni Cevin, alisema baadhi ya wazazi wanaoishi pembezoni wanawaficha watoto wao wenye ualbino na ulemavu mbalimbali kwa kuhofia kuchekwa.

Aliwataka wazazi kuacha kuwaficha watoto hao badala yake wajitokeze ili wapate elimu na kutimiza ndoto zao.

# Benki yamwaga vifaa hospitalini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HOSPITALI ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, imepokea msaada wa vifaa vya kujifungulia pamoja na sabuni kwa ajili ya wanawake wanaojifungua vyenye thamani ya Sh. milioni 1.4 kutoka Benki ya Access Microfinance Tanzania.

Akikabidhi vifaa hivyo hivi karibuni, Ofisa Mkuu wa Biashara wa Access, Isaya Mwenisongole, alisema msaada huo unalenga kuunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali katika kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto.

Msaada huo ulikabidhiwa kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Deo Nyaga.

Mwenesongole alisema wamekuwa na utamaduni wa kusaidia jamii kwa kutoa sehemu ya faida wanayoipata kama benki, hivyo wametoa vifaa vya kujifungulia wajawazito yakiwamo maboksi matano yenye vipande 18 kila moja na sabuni za unga kwa ajili ya kufualia na kila mjamzito anayefika kujifungua atakuwa akipewa.

"Msaada tuliotoa ni sehemu ya kuunga mkono jitahada za serikali katika kuboresha huduma za afya hususani kwa wajawazito ili kuendelea kupambana na vifo vitokanavyo na uzazi na watoto, kila mjamzito atakayefika hospitalini kujifungua atapatiwa sehemu ya msaada huu, " alisema Mwenisongole.

Dk. Nyaga aliishukuru benki hiyo kwa msaada wa vifaa hivyo na kusema kwamba vitawasaidia wajawazito ambao watafika hospitalini hapo kujifungua.

Alisema atahakikisha kila mmoja ananufaika na msaada huo kama sehemu ya hamasa ya kuwafanya wanawake kujifungulia katika vituo vya afya.

Dk. Nyaga alisema wodi za wanawake na watoto hususani za wajawazito zina mahitaji makubwa kulinganisha na wodi nyingine na kuwataka wadau kujitoa na kusaidia ili kupambana na vifo vitokanavyo na uzazi ikiwamo kuwahamasisha kujifungulia hospitalini badala ya kwenda kwa wakunga wa jadi.

Alisema kwa wiki wajawazito 40 hadi 60 wanajifungua kwa njia ya upasuaji na wale wanaojifungua kwa njia ya kawaida kwa mwezi ni zaidi ya 200.

Kutokana na hali hiyo, alisema wanahitaji msaada kwa kuwa mahitaji ni mengi ili kukabiliana na vifo vya uzazi.

ama
ALHAMISI JANUARI 19, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**OPERESHENI MITI MILIONI 1.5 KITAIFA ....**

**DK. Mpango aadhimisha Mapinduzi SMZ kwa upandaji maalum miti jijini Dodoma**



**Zijue ishara za nje panapo shida kwenye afya ya akili**

Ukurasa 12

# Bingwa aichambua kwikwi, tiba yake

**Na Pilly Kigome**

KWA maisha ya binadamu suala la kupata kwikwi si geni, inafahamika kuvitokea viumbe vingi vinavyoishi duniani. Ila swali je, huo ni ugonjwa?

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Watoto kutoka Hospitali ya Rufani Mkoa wa Temeke, Salha Ally, anakana kwikwi kuwa ugonjwa, bali anaitafsiri ni dalili kuna ugonjwa unataka kujitokeza kwenye mwili huo.

Anaitafsiri kwikwi inatajwa ni kitendo kisichozuilika, kitokanacho na kusinyaa kwa kuta za kiwambo cha moyo au 'diagram' kitendo kinachojirudia mara nyingi kwa mwanadamu, huku kikitoa sauti.

Dk. Ally anasema, husababishwa na kidaka tonge cha kiumbe kama binadamu (epiglottis) ambacho hufunga haraka wakati hewa inapoingia kwenye koo.

"Kwikwi pia tunaweza tukasema, ni kitendo cha kutetema au kurukaruka kwa mwili mara kadhaa, kinachotokana na hali ya mfumo wa hewa unapoingia kwenye koo hufanya hali hiyo ya kurukaruka kwa mwili," anasema.

Dk. Ally anasema, kwikwi hutokea pale upumuaji wa mtu unapositishwa kwa kipindi kifupi. Pia inaweza ikatokea bila sababu na mara nyingi huwa ya ghafla, lakini ikiendelea kwa muda mrefu ni ishara ya tatizo la kiafya.

Kwa mujibu wa daktari huyo, watu wengi hupata kwikwi na kisha inaondoka yenyewe. Pia kuna mazingira kwikwi huondoka kwa tiba za awali. Vilevile anataja, kuna kwikwi zinazochukua muda mrefu inayoendelea zaidi ya saa 48, anaitaja ni ya hatari na inahitaji msaada wa kitaalamu kutoka kwa madaktari, kwa kuwa inaendana na tatizo kubwa la kiafya.

Dk. Ally anaielezea Nipashe kuwapo kwikwi kwa mtu kila mara, maana yake ni kwamba, ana dalili ya kupungukiwa madini kama vile sodium, potassium na wengine kuangukia magonjwa ya kisukari, figo na maambukizi ya bakteria.




Mgonjwa wa kwikwi, akijipa huduma ya kwanza. **PICHA: MTANDAO**

**WATOTO WACHANGA**

Anasema, kwa upande wa watoto wachanga, hali hiyo hujitokeza kutokana na ukosefu wa maji mwilini na ikiwa mtoto hapati maziwa ya kutosha kutoka kwa mama, kuna uwezekano wa kukutana na hali hiyo ya kwikwi.

Katika hilo, anawashauri kinamama kuwanyonyesha watoto kitaalamu na kwa maelekezo maalum kutoka kwa mtaalamu wa afya, kwani kadri siku zinavyoenda, kunaonekana ukiukwaji kwa kanuni stahiki za kiafya katika kuwanyonyesha watoto wachanga, miili yao ipate mahitaji muhimu kiafya.

**INAVYOJITOKEZA, INAVYOTIBIWA**

Inatajwa pale inapotokea mtenganisho wa misuli inayoweka mipaka ya kifua na tumbo, ina mchango mkubwa katika mwendo wa mtu kupumua.

Kuna hali ya kujikunyata ghafla, sehemu ya mwanzo ya koromeo inayohusika na kutoa sauti, kwamba inajibana na kusababisha kufunguika kabisa koo. Hapo, kunachangia hewa kuingia ghafla kwenye mapafu na kutokea kwa sauti iliyozoeleka kwa jina la kitaalamu 'hic'.

Ni eneo linalohusika na sauti; kwikwi moja inaweza ikatokea au zikaja mfululizo kwa mpangilio maalum, wastani wa kwikwi mbili.

Kuna mambo yanayotajwa kuchangia ni; kula haraka haraka bila kituo, kumeza hewa pamoja na chakula, kula chakula kingi cha mafuta au chenye viungo vingi, matumizi ya vinywaji vyenye kaboni.

Mengine kwa mujibu wa Daktari Ally, kunywa pombe nyingi kwa mpigo, tumbo kujaa gesi au vidonda vya tumbo.

Anataja zingine ni mabadiliko ya ghafla ya hali ya hewa, kiharusi au uvimbe kwenye ubongo, hofu au msisimko na hata baadhi ya matumizi ya dawa zinaweza kusababisha shida kwikwi, zikiwamo zile za acid reflix, nicotine, benzodiazepines.

**UNAONDOAJE KWIKWI**

Mtaalamu wa tiba asili kutoka jijini Dar es Salaam, Hamis Kaibu, anaeleza tiba za kuidhibiti kwikwi, zinajumuisha kuweka sukari chini ya ulimi kiasi cha nusu kijiko na wakati wa kumeza, mtu abane pua kwa vidole; pili anataja kunywa maji haraka, mtu akivuta hewa taratibu kwa ndani.

Tatu, anataja kitunguuu maji nacho kinasaidia kutoweka tatizo hilo, kwa kusaga kitunguu kuchanganya na chumvi, majisafi kupatikana juisi ambayo mtu akinywa mara mbili inasaidia kukabili tatizo hilo.

Pia anataja hiliki iliyotwangwa ikichanganywa na maziwa fresh kinywaji hicho kinasaidia kuondoa tatizo hilo.

Mkazi wa Kigogo Mkwajuni, Dar es Salaam, anayejitambulisha kwa jina Saidi Selemani (57), anafafanua kuwa njia nyingine za asili zinazosaidia tatizo hilo, ni mtu kufikicha macho, kunywa maji haraka, huku akiwapo mtu kando akimwita jina lake.

Kulala usingizi kifudifudi, nako kunatajwa tiba ya tatizo hilo kwa haraka, kwa mtoto anayeweza kuwekwa begani huku akiwa anampigwa mgongoni, naye husaidiwa kwa kiwango kikubwa, kwani kunamshtukiza mgonjwa na kuondoa mwenendo wa kwikwi.

Dawa zitumikazo ni za aina nyingi na hakuna dawa maalum kwa ajili ya kutibu kwikwi. Tiba huenda zaidi kwenye visababishi.

AFYA

# Zijue ishara za nje panapo shida kwenye afya ya akili

**Na Christina Mwakangale**

KWENYE jamii masuala ya afya ya akili hususan kwa nchi zinazoendelea mwamko bado upo chini, jambo linalosababisha ongezeko la matukio, ikiwamo watu kufanyiwa ukatili kama vile kudhalilishwa nafsi zao.

Mtaalamu bingwa wa afya ya akili kutoka Idara ya Afya ya Akili, Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH), Dk. Raymond Mgeni, anasema zipo dalili ambazo kitaalamu huchukuliwa kuwa chanzo cha magonjwa hayo na hazitakiwi kupuuzwa, ikiwamo hasira, kucheka bila kuchekeshwa, kuongea bila kuwa na wa kuongea naye.

"Kukasirika kusiko na sababu au kukasirika kwa kufoka foka, pia zinaweza kuwa ni dalili ya ugonjwa wa akili. Lazima unaposema huyu ana ugonjwa wa akili, kuna vigezo huzingatiwa kutokana na miongozo ya kuleta jina la ugonjwa wa akili aliyo nayo mgonjwa," anasema bingwa.

Anaendelea: "Kupandwa na hasira ni jambo la kawaida. Hasira isiyo ya kawaida huweza kuashiria ugonjwa pia, hasa kwa ugonjwa ujulikano 'baipola'..."

Anaeleza kuwa, pia wapo watu wenye utani uliopitiliza kwa wengine, jambo linalomfanya anayetendewa utani huo kuupokea kwa mtazamo hasi au chanya, huku akionya kwamba vitendo hivyo mara kadhaa hujitokeza maeneo ambayo wamezoeana hukutana mara kwa mara kama vile maofisini.

"Mtu anataniwa na pengine anachotaniwa ni jambo la kweli. Ukishasikia kutokana na utani huo, hauwi mgonjwa, sema ni vile watu hukasirika sana wanapoguswa katika 'self-image' (mtazamo binafsi). Jinsi wanavyojitazama, ni rahisi kuathirika na maoni kutoka nje," anasema Dk. Kuganda.

Tabibu bingwa wa afya ya akili, Dk. Saidi Kuganda, anasema hata watu wanaofanya mambo mabaya, wanapoambiwa kwamba wao ndio wamefanya vitendo hivyo, hukasirika. Yote hayo, anaainisha kwamba ni muhimu jamii kuwa makini nayo.

"Watu wanaofanya mambo mabaya, wakiambiwa ukweli hukasirika. Mtu kweli ni muongo, halafu ukimwambia muongo anakasirika. 'Why'? (kwanini). Si jambo jema kutaniana kunakopeleka 'negative emotions' (hisia hasi) za mwenzio.

"Akikukataza ukatazike, ndio mtaenda sawa. Vinginevyo ni kumnyima furaha na amani mwenzio, jambo ambalo 'in a long run' (ikichukua muda mrefu) linaweza kumsababishia mwenzio hasira (negative emotion) au msongo wa mawazo.

"Hii changamoto ikizidi inaleta madhara na maradhi," anasema Dk. Kuganda, ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wataalamu wa Afya ya Akili Tanzania (MEHATA).



Anayeshukiwa kuwa na shida ya afya ya akili, wakati huo akiwa kwake: **PICHA: JARIDA UMOJA WA MATAIFA**

**USHAURI WA MABINGWA**

Dk. Mgeni, ambaye anatumikia Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), anatamkia kwamba yapo mambo muhimu 10 yanayoweza kusaidia jamii kukuza uelewa kuhusu afya ya akili na magonjwa ya akili nchini.

Hapo anaorodhesha suala la kusikiliza vipindi maalumu kupitia vyombo vya habari kama radio, runinga na maandiko magazetini.

Pia anataja haja ya mafunzo na elimu kwa jamii kuhusu afya ya akili, yanayopaswa kupewa kipaumbele mitandaoni, kwa kushirikisha wataalamu kutoka idara za afya ya akili; madaktari, wanasaikolojia, watu wa tiba kwa kazi, maofisa ustawi wa jamii pamoja wauguzi, akisisitiza hasa wa idara za afya ya akili.

"Lengo la kufanya hivi, iwe katika kutoa elimu juu ya afya ya akili na magonjwa ya akili. Jamii bado ipo gizani, inapokuja suala la afya ya akili pamoja na magonjwa ya akili. Hili linawanyima watu kupata huduma hizi haraka pindi wapatapo changamoto za kuugua akili.

"Huduma za afya ya akili na saikolojia ziwapo katika hospitali zote za serikali na taasisi binafsi. Umuhimu huu ni kuhakikisha watu wanapopata changamoto zinazoweza kuwaathiri afya ya akili, kupata huduma za wataalamu wa tiba ya akili mapema na kufikika," anasema bingwa huyo.

Hapo anafafanua nafasi ya mafunzo ya udhibiti wa msongo wa mawazo sehemu za kazi, iwe ni lazima katika taasisi za serikali na binafsi.

"Eneo la kazi limekuwa linachangia sana watu kukutana na msongo wa mawazo. Hivyo, mafunzo yanapokuwapo ya kuwajengea watu uwezo wa kukabiliana na hali za msongo wa mawazo itasaidia kupunguza changamoto za wafanyakazi wanaokuwa katika hatari ya kupata baadhi ya magonjwa ya akili mfano sonona.

"Pawe na masomo kuhusu afya ya akili na kuzifahamu dalili za makundi ya magonjwa ya akili yatakayojenga msingi kwa wanafunzi kuanzia shule za msingi, sekondari na vyuoni, namna waweze kulinda afya ya akili na pindi mtu anapokuwa na dalili aweze kujua pa kupata msaada," anashauri bingwa huyo.

Eneo lingine anataja ni haja ya kuwapo mijadala kupitia majukwaa ya mitandaoni, ikiwamo mfano 'Clubhouse, Twitter' inayogusa elimu ya afya ya akili na hatua za kuchukuliwa pindi mtu anapopata changamoto za afya akili, ajue wapi pa kwenda.

"Pawepo huduma za mawasiliano ya simu yanayopatikana wakati wote, kwa msaada wa dharura, huduma za afya ya akili pindi mtu anapofikiria kujidhuru au kutawaliwa na mawazo ya kutaka kujiua. Hili linaweza kufanikiwa kushirikiana na kampuni ya simu," anashauri mtaalamu huyo.

Dk. Kuganda anasema, pia nyumba za Ibada, iwekanisani au misikitini, viongozi wa dini wawe na nafasi ya kuwajengea uwezo waumini wao katika kudhibiti hali za hasira, ili kuepusha watu kujichukulia sheria mkononi na kudhuru wengine.

Hapo, anashauri kutolewe fursa za ufadhili kwa wataalamu wa idara ya afya ya akili, kuongeza elimu ya kibingwa kusaidia zaidi katika utoaji wa elimu na hata matibabu ya magonjwa ya akili.

Mkurugenzi wa Afya ya Akili na Matumizi ya Dawa kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO), Dévora Kestel, alihitimisha hoja ya kitaalamu, kwa kurejea Ripoti ya Afya ya Akili ya Mwaka 2022.

Kestel anasema wenye changamoto ya afya akili, hukumbana na unyanyapaa, kutengwa na jamii na mazingira duni na huduma za kusaidia afya ya akili nafuu na ubora, akisema kwamba kila mtu ana haki ya afya ya akili.



AFYA

# Safari ndefu angani inavyokaribisha maradhi mwilini mwa abiria wa ndege

**Na Tony Schiemer**



Ndege ya Shirika la Ndege la Australia, Qantas, miaka miwili ijayo inatarajiwa kuanzisha safari ya saa 19 angani, ambayo katika sura ya pili kuna changamoto ya afya ya abiria wake. **PICHA: MTANDAO**

NI hivi karibuni tu, Shirika la Ndege la Australia linalojulikana kwa jina la Qantas, limetangaza mwaka 2025 litazindua safari za ndege za moja kwa moja kutoka pwani ya mashariki ya Australia hadi London, Uingereza, ikitumia saa 19.

Ingawa ndege nyingine zina safari hadi wastani wa saa 24, lakini abiria huunganisha kwa kutua na kupaa tena. Hapo ndipo waelewa wa taaluma hiyo, wanaitafsiri 'ni safari inayogusa mabadiliko ya afya ya abiria.'

Pengine swali linalojitokeza, mwili unaweza kubadilikaje wakati wa kusafiri kwa muda mrefu? Ina tofauti na safari ndefu zilizopo za ndege zingine? Pata darasa:

**KUPUNGUKIWA MAJI**

Kunatajwa kuwapo uwezekano wa upungufu wa maji mwilini kwa abiria. Abiria anashauriwa, kabla ya kupanda ndege ya safari ndefu, ahakikishe amekunywa maji ya kutosha, licha ya ukweli kwamba upungufu wa maji mwilini ni jambo la kawaida kwenye safari za ndege za masafa marefu.

Inaelezwa ndiyo maana mtu unaweza kuhisi ukavu wa koo, pua na ngozi yake kubadilika kwenye ndege. Muda mrefu wa safari unaweza kusababisha hatari kubwa ya upungufu wa maji mwilini.

Hiyo inatokana na unyevu ikilinganishwa na ule ulio ardhini. Hiyo ni kwa sababu hewa inaingia kwenye ndege kutoka nje na hakuna unyevu mwingi katika hewa ya angani.

Mtu anaweza pia kukosa maji mwilini kwa kutokunywa maji ya kutosha, au kwa kunywa pombe kupita kiasi, kwani pombe mwilini huchangia kupoteza maji mwilini. Ushauri mkubwa wa kiafya ni mtu anaposafiri anywe maji kiwango cha ziada kabla ya kupanda ndege na wakati wa kusafiri.

**KUATHIRI UMAKINI**

Safari inatajwa inaweza kuathiri umakini wa masikio, tumbo na usingizi hata kumwachia abiria kitendawili kama anaweza kupumzika kwenye ndege?

Kijiolojia, inaelezwa kadri panapo mgandamizo kwenye ndege unavyobadilika, hewa katika mwili wa abiria nao hubadilika na hiyo inaongezeka, kadri ndege inapopanda na mgandamizo wa hewa unapungua na kinyume chake wakati ndege inashuka, ni hali inayosababisha baadhi ya matatizo ya kawaida kama vile: Maumivu ya masikio; shinikizo kwenye ngoma za masikio wakati kuna tofauti katika shinikizo la hewa kati ya ndani na nje ya ngoma za masikio.

Pia maumivu ya kichwa hutawala kwa baadhi ya watu: Hiyo kitaalamu inatajawa kusababishwa na kutanuka hewa katika mfupa mwilini na hasa ndani ya fuvu. Vilevile, kunatajwa matatizo ya tumbo, chanzo kikuu kikitajwa zaidi ni kusumbuliwa na gesi zaidi.

Mtu anaweza kuhisi usingizi zaidi kuliko kawaida; ni hali inayosababishwa na mwili kushindwa kunyonya oksijeni nyingi kutoka kwenye ndege kama ilivyo kawaida ardhini chini.

Hali hiyo inaweza kufanya mtu ahisi usingizi, lakini ni kwamba matatizo mengi si lazima yaonekane zaidi kwenye safari ndefu za ndege, mara nyingi huonekana wakati ndege inapopanda na kushuka.

**DAMU KUGANDA**

Kuna changamoto ya damu kuganda na kuziba mishipa ya damu kwa safari ndefu za ndege; mara nyingi wasiwasi mkubwa kwa abiria ni eneo hilo, kutokana na kutotembea kwa muda mrefu, athari ikianzia kwenye miguu hadi kwenye mapafu.

Inatajwa kwa waliopata uzazi karibuni au baada ya upasuaji na wamekuwa wakitumia homoni au kumeza dawa za uzazi wa mpango, kadri safari ya ndege inavyoendelea, ndivyo hatari ya kuganda kwa damu zao inavyoongezeka, kulingana na utafiti uliofanyika mwaka jana.

Watafiti walihesabu kuwa hatari ya kuganda kwa damu iliongezeka kwa asilimia 26 kwa kila saa mbili za kusafiri kuanzia baada ya saa sasa nne angani.

Pia, kuna ushahidi kwamba kuvaa soksi za kubana unaweza kusaidia kuzuia kuganda kwa damu, kwani zinatajwa kuboresha mzunguko wa damu kwenye miguu na kusaidia kurudisha damu kwenye moyo.

Kwa kawaida, hiyo hutokea kutokana na kupungua kwa misuli inayosababishwa na kutembea, ukaguzi wa kisayansi mwaka juzi iliyohusisha 2,637 katika safari zikatoa majibu hayo.

Wenye kasoro za kuganda damu, wanashauriwa kupata ushauri wa kidaktari kabla ya kuruka angani.

Kwa kawaida, mtu akiwa na damu iliyoganda, inachukua muda kuzunguka mwilini ua isizungukle.

Kwa hiyo, mtu anashahuriwa kufatilia dalili zifuatazo baada ya kusafiri: Maumivu ya mguu na uvimbe (mara nyingi mguu mmoja tu), maumivu ya kifua, kikohozi na upungufu wa pumzi na kupata usaidizi wa dharura wa matibabu ikihitajika.

**ATHARI ZA MIONZI**

Inatajwa hyaijalishi kwenye eneo lipi la abiria wa ndege, lazima asimame na atembee kila mara. Ikiwa inaruka umbali mrefu mara kila mara, inatajwa abiria anavyokaa muda mrefu angani, pia anapata zaidi mionzi ya anga.

Inatajwa mionzi kutoka angani, inaweza kuongeza saratani na hasa za uzazi, kwani haijulikani ni mionzi ipo iliyo salama. Ushauri ni kwa mjamzito ni bora kushauriana na daktari wake kabla ya kuruka angani.

Kimsingi, baadhi ya tahadhari za kawaida zinahitajika kuchukuliwa, kama vile kunawa mikono mara kwa mara, kuvaa barakoa na kutosafiri ikiwa unajisikia vibaya.

Kwa kifupi, utafiti kuhusu mwili wa binadamu unavyoweza kuguswa na safari ndefu za ndege za moja kwa moja kati ya Australia na Ulaya, bado uko katika hatua zake za awali na timu ya Australia kwa sasa inashughulikia hilo.

Hadi matokeo yawepo, ushauri wa kushughulika na safari za ndege za masafa marefu zitatangazwa. Kwa sasa abiria wanapaswa kufuata vidokezo vya shirika la ndege kama vile kumuona daktari kabla ya kusafiri, pia kunywa maji mengi, kuvaa barakoa na kudumisha tabia ya usafi, kunawa mikono kila mara.

Abiria anashauriwa kufuta matibabu ya haraka ikiwa atapata dalili zozote za kutisha baada ya safari ya ndege.

•Mwandishi wa makala hii, rubani wa kibiashara, mtaalamu wa masuala ya anga na Mhadhiri Tiba katika Chuo Kikuu cha Adelaide, Australia.

## OPERESHENI MITI MILIONI 1.5 KITAIFA ....

# DK. Mpango aadhimisha Mapinduzi SMZ kwa upandaji maalum miti jijini Dodoma

**Na Anaeli Mbise**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, anasema suala la upandaji miti linapaswa kuwa la lazima na anaagiza halmashauri zote nchini kuhakikisha zinafikia lengo la upandaji miti milioni moja na laki kwa mwaka.

Dk. Mpango anaongoza shughuli hiyo ya upandaji miti katika jiji la Dodoma katika maeneo ya Ihumwa na Msalato, ikiwa ni katika kusherehekea maadhimisho ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyofanyika wiki jana.

Anasema, miaka 59 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, yanapaswa kutumika kama chachu ya kuifanya Tanzania kuwa ya kijani na kurekebisha yale yote yaliofanyika katika kuharibu mazingira.

"Tumesisitiza upandaji miti mitatu kwa kila nyumba, walau miwili ya matunda na mmoja wa kivuli hii ni lazima tufanye tuliambiwa Dodoma ni kama jangwa hivi siyo kweli," anasema Dk. Mpango.

"Sasa nawataka wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa halmashauri na waziri ukasimamie kupanda miti sasa siyo hiari tena ni lazima," Dk. Mpango anaongeza.

Aidha, Makamu wa Rais Dk. Mpango, anasisitiza ushirikishwaji wa sekta binafsi na wafanyabiashara katika upandaji na utunzaji miti na anazisihi familia kuongeza juhudi katika upandaji miti na usafi wa mazingira.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akishiriki upandaji wa miti katika Jiji la Dodoma, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: MTANDAO.**

Anazitaka taasisi za serikali kupanda miti katika maeneo yao na kuhakikisha miti hiyo inaishi, pia akiwataka viongozi kuwa mfano katika shughuli hiyo ya upandaji na utunzaji miti kwa kuonyesha kwa vitendo.

Hapi anatoa maagizo kwa viongozi wa jiji la Dodoma, waratibu na kusimamia miti iliyopandwa, iishi na kupendezesha makao makuu ya nchi yanayopokea wageni wa ndani na nje ya Tanzania.

Anawataka kudhibiti masuala yote ya uchomaji moto maeneo yaliyopandwa miti, pamoja kukabiliana na changamoto ya uingizaji, pia upitishaji mifugo katika maeneo hayo.

Dk. Mpango anasema, kila mwananchi anawajibika kuimwagilia miti iliyopandwa, hususani wale wanaomiliki vituo vya mafuta na wanaozalisha tofali, akitoa wito kwa waandishi wa habari kutoa kipaumbele katika uelimishaji na kuhamasisha jamii juu ya upandaji miti na uhifadhi wa mazingira kwa ujumla.

Hapo inaendana na agizo lake kwa Wakala wa Misitu Nchini (TFS), kupitia upya utaratibu wa leseni za ukataji miti kwa ajili ya mkaa, ili kuokoa maeneo ambayo yana uoto na vyanzo vya maji.

**WADAU MAZINGIRA**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, anasema mipango ya uhifadhi wa mazingira imeshaanza kutekelezwa, ikiwamo kugawa maeneo yaliyopandwa miti kwa taasisi za serikali na binafsi kuzisimamia na kuhakikisha miti hiyo inaishi.

Dk. Jafo anamhakikishia Makamu wa Rais, kuwa shughuli za upandaji miti na kuitunza, itakuwa endelevu.

Mdau wa Mazingira na Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, anatoa wito kwa wananchi kuzingatia utaratibu wakati wa upandaji wa miti ikiwamo kuandaa mazingira ya upandaji na kufuata maelekezo ya wataalamu ili kufahamu aina ya mti na mahali unapopaswa kupandwa. Pinda anasema, Jiji la Dodoma linakabiliwa na upungufu wa mvua, hivyo ni vyema uchimbaji mashimo, pamoja na nafasi baina ya mti na mti ukawa wa kitaalamu zaidi, ili kuepusha miti hiyo kutofikia lengo.

Waziri Mkuu huyo mstaafu, anasema jamii ina wajibu mkubwa wa kusimamia na kutekeleza kwa makini yale yote yanayosababisha maisha ya binadamu kuwa salama ikiwamo upandaji wa miti.

Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, anasisitiza upandaji miti katika vyanzo vya maji upewe kipaumbele kimkoa, kwa kuanza na Bonde la Mzakwe ambalo limekuwa na changamoto ya ukuaji wa miti.

Senyamule anasema, wataalamu wamewezesha aina ya miti inayopaswa kupanda pamoja na kuweka mazingira yatakayookoa miti hiyo dhidi ya hatari ya moto.

"Sisi hapa kupitia ofisi ya Makamu wa Rais tunaendelea kusisitiza upandaji wa miti watendaji tutasimamia sheria kwa wale watakaoleta mifugo kula miti hii," anasema Senyamule.

Mkuu huyo wa Mkoa, anawataka walimu wa shule za msingi kuhakikisha kila mwanafunzi anapoingia darasa la kwanza apewe mti mmoja wa kuutunza hadi hapo atakapohitimu darasa la saba lengo likiwa ni kuleta mabadiliko ya tabianchi.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, anawahakikishia kushirikiana na wadau mbalimbali katika usimamizi wa upandaji wa miti pamoja na kusimamia vyema programu ya soma na mti inafanikiwa.


---

## CHEMSHABONGO NA -00 42 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. mfereji
6. kero
7. sehemu ya mbele ya kitu
8. habari
10.tunda lenye miba miba
11.aina ya ndege
12.Jiji liitwalo 305 Marekani
15.bara kubwa duniani
17.riadha 18.kwa ajili ya


Chini:
1. kitabu kitumiwacho melini kuandikia habari zake zote za kila siku
2. agiza kitu kwa mdomo
3. Injinia
4. nchi kavu 5. mwindaji
7. hali ya kupatikana kwa mafanikio
9. pinda mgongo kuelekea chini 13.Maoni 14.Ng'ata
16.hitilafu



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

SAMADI
SOMALIA
MAMALIA
MAMALISHE
DALILI
LALAMA
ITIKA: ATI
ISIMU
AKIKI: AKALI
ILI: AI: AMBO
UMA: OGA: AGA
NGEU
MADOA

maoni SMS: 0787 00 97 94



Majibu toleo lililopita







## Wadau waelekezwa malezi sahihi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WADAU wanaotekeleza mradi wa kuimarisha afya, ustawi na ulinzi kwa watoto na vijana wanaoishi katika mazingira hatarishi (USAID Kizazi Hodari), wameelekezwa kutoa elimu sahihi ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto ili kuwaandaa kuwa bora.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema hayo jana alipokuwa akizindua mradi huo jijini hapa.

Alisema pia waendeleze utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa mashauri ya watoto ili kutoa huduma kamilifu na endelevu na kuimarisha mifumo ya huduma za ulinzi na usalama wa watoto katika jamii pamoja na kushirikiana na mikoa na halmashauri kufanya ufuatiliaji wa huduma na kusimamia ubora wa takwimu.

"Mimi binafsi nitakuwa mstari wa mbele kwenda kwenye maeneo ya utekelezaji kuona maendeleo ya mradi huu. Aidha, katika kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii kwa watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi pamoja na walezi wao, wizara inaona vema afua hizo ziwekwe," alisema.

Dk. Gwajima alibainisha kuwa afua za mapambano ya ukatili wa kijinsia shuleni ni muhimu sambamba na kufanya kazi kwa umoja wa dini mbalimbali (FCI) katika kukemea na kuibua matukio ya ukatili wa kijinsia.

Alisema afua nyingine ni kuboresha na kusambaza orodha ya watoa huduma za VVU/UKIMWI, ukatili dhidi ya watoto na ukatili wa kijinsia pamoja na kuhuisha vikundi vya kiuchumi kwa ajili ya kuinua uchumi wa kaya miongoni mwa walezi na vijana balehe.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkuu wa Kanisa la Kiinjili na Kirutheri Tanzania (KKKT), Dk. Fredrick Shoo, alisema huduma hizo za kusaidia makundi ya maalum ni za msingi zinazotambulisha kanisa.

"Kanisa la KKKT limeendelea kutoa huduma hizi bila kujali dini, kabila wala itikadi," alisema.

Awali, Mkurugenzi wa Mradi wa USAID Kizazi Hodari Tanzania, Dk. Godson Maro, alisema mradi huo wa miaka mitano unalenga kuongeza utambuzi wa hali ya maambukizi ya VVU kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, kuwaunganisha na huduma za afya na uimarishaji wa huduma za usimamizi wa mashauri ya watoto.

Dk. Maro alisema mradi huo unaotekelezwa katika mikoa 12 na halmashauri 26 utaimarisha huduma za kinga, tiba na matunzo kwa watoto walioathirika na VVU na ukatili wa kijinsia.

# Kitabu usalama kazini kwa wasioona chazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amezindua kitabu maalum cha mafunzo ya usalama na afya kwa watu wasioona.

Kitabu hicho kilichoandikwa kwa maandishi ya nukta nundu, kina lengo la kuwasaidia watu hao wenye ulemavu kujifunza kanuni bora za usalama na afya mahali pa kazi.

Prof. Ndalichako alizindua kitabu hicho jana kilichoandaliwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) katika mafunzo ya siku moja ya usalama na afya kwa wasioona yaliyofanyika jijini hapa na kujumuisha wawakilishi 100.

Akizindua kitabu hicho sambamba na kufungua mafunzo hayo, Waziri Ndalichako, aliwataka kutumia kitabu hicho kwa malengo yaliyokusudiwa na serikali ili kuzingatia taratibu muhimu za usalama na afya.

"Ndugu washiriki nimefurahi kuona kwamba OSHA leo (jana) wameandaa mafunzo haya lakini jambo la muhimu zaidi katika mafunzo haya ni kwamba wameandaa kitabu maalum kilichoandikwa kwa maandishi ya nukta nundu ambayo watu wasioona wanaweza kusoma na kuelewa maudhui yaliyomo katika kitabu hicho," alisema Prof. Ndalichako.

Waziri huyo alisema serikali inaendelea kuboresha huduma mbalimbali za watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na kutunga sera, sheria, kanuni na miongozo ili kuhakikisha kuwa ustawi wa watu wenye ulemavu unazidi kuimarika.

"Pamoja na kuipongeza OSHA kwa kutambua umuhimu wa kuandaa chapisho hili kwa kushirikiana na viongozi wa vyama vya wasioona, niwaagize kuchapisha nakala za kutosha na kuzisambaza kwa makundi mengine zaidi sambamba na kuendelea kutoa mafunzo hayo muhimu sana kwa kila mfanyakazi kutegemeana na shughuli anazozifanya," alisema.

Naye Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema wameandaa chapisho hilo na mafunzo ikiwa ni utekelezaji wa jukumu la taasisi linalowataka kutoa elimu ya usalama na afya kwa makundi mbalimbali katika jamii wakiwamo watu wenye ulemavu.

"Sisi OSHA tunatambua kwamba ulemavu ni hali tu ambayo hawaondolei utu watu wenye ulemavu wala nafasi yao ya kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi hivyo tunayo programu maalum ya kuyawezesha makundi mbalimbali wakiwamo watu wenye ulemavu kufanya kazi zao za kila siku katika hali ya usalama na afya.

"Hivyo tumekuwa tukitoa mafunzo kwa makundi mbalimbali wakiwamo wachimbaji wadogo, wakulima, mamalishe, mafundi pamoja na watu wenye ulemavu kama tutakavyofanya kwa kundi hili la watu wasioona ambalo tumekwenda mbali zaidi kwa kuwaandalia kitabu maalum cha mafunzo," alisema.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wasioona Tanzania, Omary Itambu, aliishukuru OSHA kwa kutilia mkazo suala la uwezeshaji wa watu wenye ulemavu hususan wasioona.

"Tunaishukuru OSHA kwa jitihada inazofanya katika kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu hawaachwi nyuma katika masuala haya ya usalama na afya. Nasi tunaahidi kuitumia vema nafasi hii ambapo tutayazingatia yote wanayotufundisha na hivyo kuweza kuzalisha kwa tija kwa maendeleo endelevu ya taifa letu," alisema.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Doroth Gwajima, akifurahia jambo na Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Fredrick Shoo, baada ya kuzindua rasmi mradi wa USAID Kizazi Hodari, jijini Dodoma juzi, wenye lengo la kusaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi na utatekelezwa kwenye mikoa 12 nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mradi uboreshaji usalama milki ardhi waanza

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeanza kutekeleza mradi wa uboreshaji usalama wa milki za ardhi nchini (LTIP), unaotarajia kutoa hati miliki na leseni za makazi milioni 2.5 ili kuboresha usalama wa ardhi kwa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa wananchi.

Mradi huo unafadhiliwa na Benki ya Dunia kwa gharama ya Sh. bilioni 345 na utekelezaji wake ni wa kipindi cha miaka mitano.

Akifungua mkutano wa kitaifa wa kujadili utekelezaji wa mradi huo jana jijini hapo, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, alisema mradi huo unaenda kutekelezwa katika halmashauri 41 katika mikoa 16 nchini, hivyo kuhimiza uadilifu katika utekelezaji wake.

"Umakini na uzalendo unahitajika katika utekelezaji wa mradi huu na mradi huu utatumiwa na Benki ya Dunia kupima uwezo wa Tanzania katika kutekeleza miradi ya ardhi," alisema. Alitoa angalizo kwa wananchi kujiepusha na migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali hapa nchini kutokana na kuwapo na ongezeko la watu.

Ridhiwani alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazokabiliwa na kasi kubwa ya ukuaji wa miji na vijiji kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu linalosababisha kuongezeka kwa mahitaji ya ardhi yaliyopangwa ambayo usimamizi mzuri na salama.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Allan Kijazi, alisema mradi huo ulitiwa saini na Benki ya Dunia Januari 21, mwaka jana na utatoa hati miliki milioni moja, leseni za makazi milioni moja katika maeneo ya mijini na hati za hakimiliki za kimila 500,000.

Alitaja inayotekelezwa mradi huo kuwa ni Pwani, Simiyu, Iringa, Tanga, Tabora, Geita, Kigoma, Mara, Shinyanga, Dodoma, Mbeya, Kilimanjaro, Ruvuma, Songwe, Katavi na Arusha.

Mwakilishi wa Benki ya Dunia, Nicholaus Saikani, alisema mradi huo wanauangalia sana kutokana na umuhimu wake.





# Wananchi wadaiwa kuhujumu mpaka Hifadhi ya Ruaha

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

BAADHI ya wananchi wa Kata ya Imalilo-Songwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wanadaiwa kuhujumu mpaka mpya wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na maeneo ya wananchi kwa kung'oa alama zilizowekwa na serikali.

Alama hizo zinawekwa ili kuainisha mipaka mipya baada ya serikali kurekebisha mipaka kwa kuviacha vijiji 34 kati ya 39 ambavyo kwa mujibu wa Tangazo la Serikali namba 28 (GN 28) ya mwaka 2008 vilikuwa vinadaiwa kuwa viko ndani ya hifadhi hiyo na vilitakiwa kuondolewa.

Tangazo hilo lilisababisha mgogoro baina ya wananchi na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) ambao umedumu kwa zaidi ya miaka 15 na kuathiri shughuli za maendeleo zikiwamo kilimo, ufugaji na shughuli za uhifadhi.

Mwenyekiti wa kamati ya mawaziri nane wa kisekta waliokuwa wanashughulikia mgogoro huo, Dk. Angelina Mabula aliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya Waziri Mkuu katika Kata ya Itamboleo iliyokuwa na lengo la kuwaeleza wananchi kilichofanywa na serikali.

Mabula ambaye ni Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi alisema baadhi ya wananchi hao wamekuwa waking'oa alama zinazowekwa na maofisa wa serikali kwa nia ya kuhujumu utaratibu wa kurekebisha mipaka.

Aliwataka wananchi hao kuacha tabia hiyo kwa maelezo kuwa inaharibu nia njema ya serikali ya kuwasaidia kumaliza mgogoro huo ambao ulikuwa unasumbua kwa muda mrefu.

"Waling'oa alama hizo mara ya kwanza maofisa wetu wakazirejesha lakini wakang'oa tena, naomba wananchi muwe walinzi wa alama hizo kwa sababu zimewekwa kwa lengo la kuwasaidia wenyewe," alisema Dk. Angelina.

Alisema kutokana na mgogoro huo kudumu kwa muda mrefu, mawaziri kwa kushirikiana na wataalamu walipiga kambi kwenye eneo hilo na wakaumaliza kwa kurekebisha mipaka.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana, aliwataka wananchi wa vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo kuacha kufanya shughuli zozote za kibinadamu ndani ya hifadhi ili kupisha shughuli za uhifadhi kuendelea bila kuzua migogoro.

Alisema shughuli ambazo zimekuwa zikichangia zaidi uharibifu wa mazingira kwenye hifadhi hiyo ni ufugaji na kilimo kwa maelezo kuwa baadhi ya wafugaji wamekuwa wakiingiza mifugo hifadhini huku baadhi ya wakulima kuchepusha maji bila utaratibu.

Alisema kwa mujibu wa sheria ni kwamba mifugo inayokamatwa hifadhini inatakiwa kutaifishwa ili kufidia uharibifu unaokuwa umefanyika pamoja na kutoa somo kwa wafugaji wengine wanaokuwa na nia ya kuchunga mifugo ndani ya hifadhi.

"Tumekuwa tukikamata mifugo mingi sana ndani ya hifadhi, sasa naomba wananchi mliopo hapa mtusaidie kufikisha ujumbe kwa wenzenu kuwa mifugo hiyo itataifishwa," alisema Dk. Chana.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema baada ya mipaka ya hifadhi hiyo kurekebishwa, wizara itafanya utaratibu wa kuvisajili upya vijiji vyote vilivyoguswa na mabadiliko hayo.

Alisema watashirikiana na wizara zingine kushughulikia kero zote za wananchi wa maeneo hayo ili kuhakikisha wananchi wanaendelea kuishi kwa amani na kufanya shughuli za uzalishaji mali kwa amani.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashidi Chuachua, akipanda mti kwenye eneo la skimu ya umwagiliaji Bonde la Uyole jijini Mbeya jana, wakati wa kuzindua upandaji miti kwenye kingo za Mto Igawilo ili kuzuia mmomonyoko. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Serikali, wananchi wapanda miti kudhibiti mmomonyoko ardhi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI wilayani Mbeya kwa kushirikiana na wananchi wa Bonde la Uyole, imeanza kupanda miti kwenye kingo za Mto Igawilo ili kudhibiti mmomonyoko wa ardhi na mafuriko ambayo yamekuwa yakiathiri makazi ya watu.

Mto huo ni ule ambao wiki mbili zilizopita ulihama njia na kuvamia makazi ya wananchi ambapo zaidi ya kaya 400 ziliathirika pamoja na miundombinu ya barabara kuharibiwa hasa katika maeneo ya Uyole na Nsalaga.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, jana aliungana na wananchi wa Bonde la Uyole pamoja na maofisa mbalimbali wa serikali kupanda miti katika eneo hilo ambalo mto umekuwa ukihama njia.

Akizungumza baada ya kupanda miti hiyo, Dk. Chuachua aliwataka wananchi wa maeneo yote ya wilaya hiyo kupanda miti kwenye maeneo yao ili kutunza mazingira.

Aliwataka wakulima wa Skimu ya Umwagiliaji ya Bonde la Uyole kuhakikisha wanaitunza miti hiyo ili idumu na isaidie kudhibiti mmomonyoko wa ardhi pamoja na kudhibiti mkondo wa mto huo kuhamahama.

Alisema baadhi ya wananchi wamekuwa wakipanda miti kwenye mashamba yao lakini baada ya muda mfupi wanaing'oa kwa sababu ambazo hazijulikani na hivyo akaagiza wadhibitiwe.

"Nakutaka Mwenyekiti wa Skimu hii pamoja na viongozi wenzako mhakikishe miti hii inatunzwa, mtu yeyote atakayeharibu miti hii achukuliwe hatua za kisheria ili kukomesha tabia hii, haiwezekani tunatumia gharama kubwa kupanda miti lakini watu wahujumu," alisema Dk. Chuachua.

Alisema kitendo cha mto huo kuhama njia kimekuwa kikisababishwa na uharibifu wa mazingira ambao umekuwa ukifanywa na wananchi wa maeneo hayo hasa kilimo kisichokuwa endelevu pamoja na ukataji wa miti.

Mwenyekiti wa Skimu ya Umwagiliaji ya Bonde la Uyole, Maneno George, alisema watahakikisha wanapanda miti yote waliyopelekewa na serikali ya wilaya hiyo ili iwasaidie kuzuia korongo la mto huo kuendelea kupanuka.

Alisema mafuriko yaliyotokea hivi karibuni na kuathiri makazi ya watu yaliathiri pia mashamba yao kwa baadhi ya maeneo kufunikwa na maji na hivyo kusababisha hasara kwao.

Alisema baada ya kupanda miti hiyo watahakikisha wanailinda kwa kushirikiana na viongozi wa kata na mitaa ili idumu na kuwasaidia kwa muda mrefu kuzuia mafuriko.

"Kama mnavyoona hili korongo la mto linaendelea kukua kutokana na mto huu kuanza kumeza mashamba yetu, kwa hiyo tunamshukuru Mkuu wa Wilaya kwa kutuletea miti hii na tumhakikishie kwamba tutaipanda na kuilinda ili ikue," alisema Maneno.

# Serikali yaanza upya usanifu wa ujenzi Bwawa la Rwanyo

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI imeanza usanifu mpya wa ujenzi wa Bwawa la Rwanyo lililoko Igurusi wilayani Mbarali ambalo ujenzi wake ulisimama kwa zaidi ya miaka 10 baada ya kukumbwa na tuhuma za ufisadi likidaiwa kujengwa chini ya kiwango.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, jana alitembelea bwawa hilo na kuagiza usanifu wake uanze upya ili serikali ilikamilishe na litumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

"Serikali inatambua kuwa ujenzi wa bwawa hili ulikumbwa na mambo mengi, ikiwamo tuhuma za ubadhirifu wa fedha, lakini wakati wahusika wakiendelea kushughulikiwa na vyombo vya dola, sisi tumeamua tuanze upya ujenzi wa bwawa hili ili lihudumie wananchi," alisema Mavunde.

Alisema katika kipindi cha mwaka huu wa fedha bwawa hilo litafanyiwa upembuzi yakinifu ili kutambua gharama za ujenzi na mwaka ujao wa fedha litatengewa bajeti kwa ajili ya kujengwa.

Mkurugenzi wa Tume ya Umwagiliaji nchini (NIRC), Raymond Mdolwa, alisema utafiti wa awali uliofanyika ni kwamba bwawa hilo litajengewa kingo mpya na kuongezewa kina ili liweze kuhifadhi maji yatakayohudumia wakulima wengi zaidi katika kilimo cha umwagiliaji.

"Bwawa hili litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kuhudumia skimu tatu za umwagiliaji zilizoko katika eneo hili la Igurusi na hata kule ng'ambo ya barabara kuu, hii ni kwa sababu utafiti tulioufanya unaonyesha tutalijenga kisasa ili liwe na uwezo wa kuhifadhi maji mengi zaidi ya namna lilivyosanifiwa awali," alisema Mdolwa.

Alisema kwa namna bwawa hilo litakavyojengwa, wakulima walio jirani watajengewa mifereji ya kawaida ya umwagiliaji itakayoelekezwa kwenye mashamba yao na wale walio ng'ambo ya barabara watawafikishia maji kutoka kwenye bwawa hilo kwa kutumia mabomba.

Diwani wa Kata ya Igurusi, Hawa Kihwele, alisema ujenzi wa bwawa hilo utakuwa ni mkombozi wa wananchi wote wa kata ya Igurusi na maeneo jirani kwa kuwa watakuwa na uhakika wa kupata maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na pia kwa matumizi ya nyumbani.




Mrakibu wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar (MAGEREZA), Salum Msabaha, akizungumza katika kikao cha uwasilishaji wa taarifa kuhusu takwimu za makosa ya jinai, madai na jinsia katika ofisi ya mtakwimu mkuu wa serikali, Mazizini jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Muswada wa faragha kwa wafungwa waandaliwa Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Magereza (Zanzibar) linatarajia kupeleka Muswada wa Haki ya Kukutana na Wenza kwa wafungwa walioko gerezani katika Wizara ya Sheria na Katiba, ambao utatoa fursa kwa wanandoa kukutana kimwili.

Hayo yalielezwa na Mrakibu wa Magereza Zanzibar, Salum Msabaha, wakati akizungumza na Nipashe kuhusiana na malengo ya muswada huo ambao umeibua mjadala miongoni mwa wanaharakati na wananchi.

Mahojiano kati ya Nipashe na Msabaha yalifanyika muda mfupi baada ya kufanyika kwa mkutano wa uwasilishaji wa utoaji wa takwimu za makosa ya jinai, madai na jinsia kwa mwaka 2022.

Alisema wamejifunza kutoka nchi mbalimbali kama Kenya, China na Afrika Kusini, kwamba kwa nchi kama Afrika Kusini, sheria inaruhusu wanandoa kutembelea wafungwa na kukutana kimwili, kwamba wafungwa wao wanaruhusiwa kuagiza makahaba.

"Sisi tumewalenga wanandoa pekee, ambapo kutakuwa na chumba cha faragha kwa ajili ya wanandoa kukutana," alisema Msabaha.

Mswada huo umekuja baada ya wafungwa kuiomba serikali kutoa fursa kwa wanandoa kukutana na wenza wao wanaotumikia vifungo magerezani.

Akizungumzia madai ya kuwapo kwa vitendo vya ushoga katika magereza alisema tuhuma hizo hazina msingi kwa sababu wafungwa na watuhumiwa hupimwa mara kwa mara ili kubaini tabia zao. Ofisa Mfawidhi kutoka Tume ya Haki za Binadamu, Sada Ahmed Massoud, alisema tume inaunga mkono muswada huo na kwamba utasaidia kupunguza matatizo ya ndoa ikiwamo kupunguza talaka.

Alisema wafungwa wanapokuwa na matamanio wanaweza kuvunja haki za binadamu kwa watu wengine hivyo kupitishwa kwa muswada huo kutatoa fursa kwa wafungwa kupunguza matamanio yao kimwili.

Alisema tendo la ndoa kwa wanandoa ni haki ya msingi ya binadamu na wanapokoseshwa haki hiyo ni uvunjifu wa haki za binadamu.

"Miongoni mwa sababu zinazosababisha kuvunjika kwa ndoa ni vifungo gerezani na mmoja wa mwanandoa anapofungwa uvumilivu huondoka na talaka hutoka, hivyo miswaada huo utapunguza wimbi la talaka," alisema. Aidha, aliwataka wanandoa endapo muswada huo utapitishwa kutoona aibu na kuitumia haki yao hiyo ya msingi ili kudumisha ndoa zao.

Mkurugenzi wa Jinsia, Siti Abasi Ali alisema hatua hiyo itapunguza kasi ya matamanio ya kimwili kwa wafungwa hivyo ni vyema muswada huo ukapitishwa.

# Kilimo cha nazi Zanzibar chaanza kupotea

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo, Sahamata Shaame Khamis, amesema kilimo cha nazi Zanzibar kimeanza kudidimia kutokana na kupungua kwa uzalishaji wa miti ya zao hilo.

Amesema hali hiyo imesababisha Serikali ya Zanzibar kuagiza miti ya zao hilo nchi jirani ikiwamo Kenya, Mafya na Tanga kwa Tanzania bara.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kuhusu matatizo yaliyoko katika zao hilo.

Alisema takwimu za sensa ya miti ya mwaka 2013 Zanzibar zinaonesha kwamba miti ya minazi imepungua kutoka milioni 5.7 iliyokuwapo mwaka 1993 hadi miti milioni 3.5 mwaka 2013.

Alisema hali hiyo ni ya kutisha na imesababisha serikali kuweka mikakati maalum ya kulinusuru zao hilo kwani ni kiungo muhimu kwa utamaduni wa Zanzibar.

Alisema licha ya juhudi nyingi zilizochukuliwa na serikali lakini hali ya uzalishaji wa nazi bado sio nzuri.

"Takwimu zinatuonesha kwamba eneo la kilimo cha minazi limepungua kutoka hekta 22,000 mwaka 1997 hadi hekta 16,898 kwa mwaka 2013,"alisema.

Shamata alisema uzalishaji wa nazi nao umepungua kutoka nazi milioni 119,747,200 mwaka 1997 hadi nazi milioni 79,807,200 mwaka 2013.

Alizitaja sababu kuu ya kupungua kwa uzalishaji wa nazi ni kasi ndogo ya uoteshaji na uhudumiaji wa minazi, wizi wa nazi shambani, biashara ya madafu isiofuata taratibu na ukataji holela wa miti ya minazi.

Waziri Shamata alisema uzalishaji mdogo wa nazi umesababisha bei za zao hilo kupanda na taarifa zinaonesha kwamba mwaka 2012 wastani wa bei ya nazi moja ilikua ni Sh. 400 na mwaka 2022 wastani wa bei ya nazi moja Sh. 1,500.

Alisema: "Hali hii imesababisha kuongezeka kwa uingizwaji wa nazi kutoka Tanzania Bara ambapo wastani wa nazi 126,000 huingizwa katika Kisiwa cha Unguja kwa mwezi".

Aidha, alisema zao hilo kwa kipindi kirefu limesaidia uchumi wa nchi, kwamba Zanzibar ilikuwa msafirishaji mkubwa wa mazao yatokanayo na mnazi ikiwamo mbata, mafuta ya nazi pamoja na bidhaa zitokanazo na usumba kama vile mazulia na kamba.

"Lakini kutokana na kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya nazi kulikotokana na kuzeeka kwa minazi yetu na kukatwa kwa kiwango kikubwa kwa ajili ya makazi, samani, kilimo na kushamiri kwa biashara ya madafu kumesababisha kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya mnazi na hatimaye kulazimika kuagiza nazi kutoka nje ya visiwa vyetu,"alisema Shamata.

Alisema serikali imedhamiria kuandaa mpango maalum wa kufufua zao la nazi kwa kuongeza uzalishaji, usarifu na matumizi endelevu ya zao la nazi.

Alisema pia serikali inakusudia kuweka utaratibu wa kuhifadhi, kudhibiti na kushajiisha matumizi sahihi wa nazi na kwamba hawataruhusu minazi ikatwe kiholela kwa ajili ya mbao wala kuruhusu minazi iliyowekwa kwa ajili ya uzalishaji wa nazi kutumika kwa ajili ya madafu.

Akizungumzia kuhusu biashara ya madafu alisema ni tatizo kubwa katika uzalishaji wa nazi na inakisiwa ya kwamba hadi madafu 3,000 huuzwa kwa siku Zanzibar.

# Serikali kula sahani moja na wanaowatelekeza watoto

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imesema haitamfumbia macho mtu yeyote anaendelea kuwatelekeza watoto na wanaotenda vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Waziri wa wizara hiyo, Riziki Pembe Juma alisema hayo jana wakati wa sherehe maalumu ya uzinduzi wa Kituo cha Mafunzo ya Amali cha Assalaam, kilichoko Kizimkazi Mkunguni Mkoa wa Kusini Unguja kilichoanzishwa na Hatice C, kutoka nchini Uturuki.

Alisema serikali itaendelea kupambana na watu hao kama sheria, sera pamoja na miongozo inavyoeleza juu ya matendo hayo.

Alisema wizara inaendelea kufanya marekebisho ya Sheria ya Mtoto Namba 6 ya mwaka 2011, ikiwa ni miongoni mwa malengo yake ya kupambana na watu hao, kwa kuwaweka watoto katika mazingira mazuri na salama.

Aidha, aliwataka wanawake wajane waliomaliza masomo yao ya amali katika kituo hicho, kujiendeleza kwa kujiunganisha vikundi ili kuwe na urahisi katika kuwapatia mikopo au midaada pale inapotokezea kwa lengo la kuwainua kiuchumi.

Aliwataka kutambua kuwa ujane siyo sifa wala siyo njia ya kujipatia fedha kwa kuomba, bali ni kuwa imara katika kujitetea haki zao.

Mkuu wa Kituo cha Mafunzo ya Amali cha Assalaam, Adnan Issa, alisema kituo hicho kimeanzishwa mwaka 2017 kwa kuwa na wanawake wajane 42 kutoka Wilaya ya Kusini lakini hadi sasa ni wanafunzi 30 tu ndiyo wamemaliza na wingine kuendelea kutokana na sababu mbalimbali.

Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja, Rajab Mkasaba, alisema kuanzishwa kwa kituo hicho kunatokana na uongozi thabiti wa Rais Dk. Mwinyi katika kuruhusu wawekezaji kuwekeza nchini ili kusaidia huduma mbalimbali za kijamii.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LARGI FIDEUS KYORO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAV4** yenye usajili namba **T 541 DFR,** CHASSIS NAMBA: **ZCA260022359** na ENGINE NAMBA: **1ZZ0832332.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/KIM/RB/24313/2023**

## KUPOTEA KWA VYETI



ESPERANSA NICOLAUS ANATANGAZA KUPOTEA KWA VYETI VYAKE, CHETI CHA ELIMU YA SEKONDARI CHENYE INDEX NUMBER P. 1616-0013 KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI TANZANIA (NECTA) KUPITIA KITUO CHA MTIHANI CHA VICTORIA I. A. E. CENTRE 2008, CHETI CHA CHUO CHA UALIMU CHENYE INDEX NUMBER E0516-0032 KILICHO TOLEWA NA NECTA KUPITIA CHUO CHA UALIMU MURUTUNGURU TEACHERS' COLLEGE 2011.

KWAYEYOTE ATAKAYEVIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU NAE: MWA/MIS/RB/14548/2023 AU APIGE SIMU NAMBA: 0769664552.

## KUPOTELEWA NA CHETI



**FIGHTER GERALD MWAGALA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S1267/0024** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **BROOKEBOND SEKONDARI** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MSI/RB/301733/2022.**

## HATI YA KIAPO CHA KUBADILI MAJINA

Mimi **YUSUFU DAVID SALU** umri miaka 60, kabila Mnyakyusa, Mkazi wa Magomeni, Mkoa wa Dar es salaam, Dini Mkristo, nikiwa na akili zangu timamu na bila kushawishiwa na mtu yeyote naapa na kuthibitisha mbele ya Mahakama hii kwamba:-

1. Mimi nimekuwa ninatumia majina matatu tofauti ambayo ni **YUSUFU DAVID SALU, YUSUFU MWAKIPESILE na YUSUFU SALU MWAKIPESILE.**
2. Kwamba, baadhi ya nyaraka zangu zilizobeba majina hayo ni pamoja na kitambulisho changu cha Taifa, kadi yangu ya kura, nyaraka zangu za PSSSF na Benki.
3. Kuanzia leo hii naacha rasmi kutumia majina mawili kati ya hayo, yaani **YUSUFU MWAKIPESILE na YUSUFU SALU MWAKIPESILE** ambayo hasa yapo kwenye nyaraka zangu za PSSSF na Benki. Badala yake nijulikane kwa jina la **YUSUFU DAVID SALU.**
4. Kwamba nimeamua kutumia jina hilo la YUSUFU DAVID SALU kwa sababu ndilo jina lililopo kwenye nyaraka zangu nyingi za Msingi, ikiwemo kitambulisho changu cha Taifa.

   Nazidi kusisitiza kwamba kuanzia leo hii mahali popote nitambulike kwa jina **YUSUFU DAVID SALU badala ya YUSUFU MWAKIPESILE** na **YUSUFU SALU MWAKIPESILE,** na endapo itagundulika vinginevyo hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yangu mtoa tamko hilo.

........................
Sahihi ya mtoa kiapo

Kwa kuwa mtoa kiapo hiki ni mtu mzima na mwenye akili timamu nathibitisha kiapo chake leo hii.

Imeshuhudiwa na;

JINA: T. CHOLAMILA

CHEO: HAKIMU — HAKIMU MKAZI

SAHIHI: ........ MAHAKAMA YA MWANZO MAGOMENI - KINONDONI

TAREHE: 17/01/2023



## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

**THE COMPANIES ACT, 2022**
**(Section 334)**

**NAWNAW MODERN CATERING LIMITED**
**(COMPANY NO. 151753302)**

**MEMBERS VOLUNTARY WINDING UP**

**NOTICE IS HEREBY GIVEN** to the General Public that **NAWNAW MODERN CATERING LIMITED** a Company with Registration Number 151753302 dully convened a meeting on 8th December, 2022 and passed a special resolution in accordance to section 333 (1)(b) of the Companies Act, 2002 that a Company be wound up voluntarily.

**ALL PARTIES CONCIRNED** and who have claims are hereby notified to submit their claims in a closed envelop within 30 days to **PHILEMON MSEGU** (Esq) of Plot No. 348 Block "A" CBD Area Kibaha P. O. Box 30296 Kibaha who is appointed liquidator of the Company.

Any Claims lodged after 30 days from this publication will not be considered for admission.

PHILEMON MSEGU (Esq)
Liquidator
For NAWNAW MODERN CATERING LIMITED

---

**3FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 1218 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late REMISTONE RAMSAY KISANGA**
**and**
**In the Matter of Application for Letters of Administration by**
**VICTORIA REMISTONE KISANGA AND RAMITHANKS RAMSAY KISANGA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 7 day of March, 2023.

Dated at DAR ES SALAAM this 17 day of January, 2023.

........................
Senior Resident Magistrate

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......07/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: RICHARD LEWANGA MASSAWE WA PNGAWE**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA PROF.APIA WILBARD MASSAWE**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 20 Mwezi 01 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 17 mwezi 01 mwaka 2023

**HAKIMU MFAWIDHI**

........................
HAKIMU

---


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Watanzania 3 waokolewa baharini Kenya

**NAIROBI,** KENYA

WAVUVI watatu wa Tanzania wameokolewa na meli ya mizigo baada ya kukwama baharini kwa siku tatu na kuwasili salama katika Bandari ya Mombasa Jumanne usiku.

Polisi wanasema kuwa watatu hao wanatoka eneo la Tanagani Pemba na walinusurika bila chakula wala maji baada ya mtumbwi wao waliokuwa kwenye msafara wa uvuvi kupinduka kutokana na dhoruba kali.

"Matumaini yao ya kurejea kwa familia zao wakiwa na samaki wengi yaligeuka kuwa ndoto, kwani watatu hao walitumia zaidi ya saa 55 kwenye bahari kuu wakicheza mchezo wa paka na panya na papa na viumbe wengine hatari ili kuokoa maisha yao," Ofisi ya Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) ilisema.

"Kimiujiza, watatu hao walipambana na dhoruba na upepo mkali zilizosababishwa na mawimbi ya monsuni ya kaskazini mashariki na kufanikiwa kukamata meli, ambayo walielea juu ya maji kwa mara nyingine na kuruka ndani," walisema polisi.

"Balozi ya Tanzania iliarifiwa mara moja na baada ya watatu hao kuhojiwa, alibaini kuwa walikuwa raia wa Tanzania," polisi walisema, na kuongeza kuwa mipango inaendelea kuhakikisha kwamba wanarejeshwa nyumbani. **BBC**

**"Kimiujiza, watatu hao walipambana na dhoruba na upepo mkali zilizosababishwa na mawimbi ya monsuni ya kaskazini mashariki na kufanikiwa kukamata meli, ambayo walielea juu ya maji kwa mara nyingine na kuruka ndani," walisema polisi.**

# UN yashinikiza haki za wanawake Afghanistan

**KABUL,** AFGHANISTAN

WAJUMBE wa ngazi ya juu katika Umoja wa Mataifa (UN) akiwamo mwanamke aliye na cheo cha juu zaidi katika umoja huo, Amina Mohammed, wamewasili Kabul Afghanistan kushinikiza haki za wanawake na wasichana.

Hatua hiyo ni jibu la matukio ya hivi karibuni ya watawala wa Taliban kukandamiza haki za wanawake, wasichana na waandamanaji.

Naibu Katibu Mkuu wa UN, Amina Mohammed, ambaye ni waziri wa zamani nchini Nigeria, ameongozana na Sima Bahous, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Haki na Masuala ya Wanawake katika umoja huo kwenye ziara hiyo.

Hayo yamesemwa na Naibu Msemaji wa Umoja wa Mataifa, Farman Haq, alisema kuwa ofisa mwengine katika ujumbe huo ni Khaled Khiari ambaye ni Katibu Mkuu Msaidizi wa UN anayeshughulika na masuala ya siasa.

Haq alisema hawezi kutoa taarifa kamili kuhusu ratiba zao au mikutano haswa watakayofanya wakiwa Kabul, kwa sababu za kiusalama.

"Maofisa wa UN wamekuwa wakifanya misururu ya mashauriano ya ngazi ya juu kote eneo la Ghuba, barani Asia na Ulaya, kuhusu hali ya Afghanistan, kwa lengo la kukuza na kulinda haki za wanawake na wasichana kuishi kwa amani na maendeleo endelevu," alisema Haq.

Kabla ya kuwasili mjini Kabul, maofisa wa ujumbe huo walikutana na viongozi wa nchi 57, ambao ni wanachama wa Ushirikiano wa Mataifa ya Kiislamu.

Kwa mujibu wa Haq, ujumbe huo pia ulikutana na maofisa wa Benki ya Maendeleo ya Kiislamu, makundi ya wanawake wa Afghanistan walioko Ankara, Uturuki na Islamabad, kundi la mabalozi na wajumbe maalum wanaowakilisha mataifa yao nchini Afghanistan lakini ambao wako Doha, mji mkuu wa Qatar.

"Kote walikozuru, nchi na washirika mbalimbali walitambua juhudi muhimu za UN, katika kutafuta suluhisho la kudumu na haja ya kuendelea kutoa misaada ya kuokoa maisha Afghanistan na walitaka juhudi hizo kuimarishwa ili kuakisi haja ya dharura iliyoko," alisema Haq.

Alieleza kuwa ziara hiyo imejiri wakati mashirika yasiyopungua matatu ya kimataifa yameanza tena kusambaza msaada wa kiutu nchini Afghanistan, baada ya kuhakikishiwa na utawala wa Taliban kuwa wanawake wanaweza kuendelea kufanya kazi katika sekta ya afya.

Mashirika ya CARE, Save the Children na International Rescue Committee yaliahirisha shughuli zao mwezi Desemba 2022 kupinga hatua ya serikali mjini Kabul kupiga marufuku wanawake kufanya kazi katika mashirika ya msaada.

Shirika la 'Save the Children' limethibitisha katika taarifa yake kuwa limeanzisha tena shughuli zake kutokana na hakikisho la Taliban. **DW**



Wanawake wa Afghanistan wakiandamana kupinga marufuku ya serikali dhidi yao kupata elimu ya vyuo vikuu. **PICHA: MTANDAO**

# Polisi aliyemuua Floyd ataka kesi ifutwe

**WASHINGTON,** MAREKANI

OFISA wa polisi Derek Chauvin (46) ambaye alimuua Mmarekani mwenye asili ya Afrika George Floyd na kuibua hasira kubwa nchini Marekani mwaka 2020 anajaribu kuomba ili hukumu yake ya mauaji ifutwe.

Chauvin, alipatikana na hatia ya mauaji na mahakama ya kaskazini mwa jimbo la Minnesota kutokana na kesi inayomkabili na ambayo iligonga vichwa vya habari mwaka 2021 na kuhukumiwa kifungo cha miaka 22 na nusu jela.

Inaelezwa kuwa polisi huyo anaamini kwamba haki zake katika kesi isioegemea zimekiukwa, hasa kutokana na utangazaji kuhusu kesi hiyo na vitisho vya vurugu ambavyo vilisababisha mabadiliko ya kimazingira wakati kesi hiyo ilipokuwa ikisikilizwa mahakamani na kutaka uamuzi huo ufutiliwe mbali. Licha ya maombi hayo, Chauvin atasalia gerezani kwasababu alikiri hatia ya ukiukaji wa haki za kiraia kwa George Floyd mbele ya jaji wa shirikisho na akapokea hukumu ya mwisho ya miaka 21 jela mwaka 2022.

Aidha, Mei 25, 2020, ofisa huyo wa polisi wa Minneapolis, ambaye alikuwa akihudumu kwa miaka 19, alipiga goti juu ya shingo ya marehemu Floyd kwa karibu dakika kumi, bila kujali kelele za wapita njia waliojawa na hofu.

Tukio hilo, lililorekodiwa na kuchapishwa mtandaoni, lilizua maandamano makubwa dhidi ya ubaguzi wa rangi na ukatili wa polisi kote Marekani na kwingineko duniani.

Wakati wa kesi katika mahakama ya eneo hilo, wakili wake aliomba kwamba Floyd alikufa kutokana na matumizi ya nguvu ya kiasi, pamoja na matatizo ya kiafya na akahakikisha kwamba Chauvin alitumia nguvu.

Licha ya hayo yote ofisa huyo wa zamani wa polisi anatafuta kubatilisha kesi hiyo, haswa kwasababu ilifanyika katika miji pacha ya Minneapolis-Saint-Paul, ambayo ilikuwa bado iko ukingoni chini ya mwaka mmoja baada ya mkasa huo. **RFI**

# GEITA GOLD KAMILI KUIVAA POLISI TANZANIA KESHO

Na Shufaa Lyimo

BENCHI la ufundi la Klabu ya Geita Gold limesema limejipanga vizuri kwa ajili ya mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya timu ya Polisi utakaopigwa kesho Ijumaa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fred Minziro alisema wachezaji wote wanaendelea vizuri kuelekea kwenye mchezo huo ambao amekiri kuwa utakuwa na upinzani mkubwa.

"Tumejiandaa kukutana na timu ya Polisi na tumeupa umuhimu mkubwa mchezo huo licha ya kwamba wapinzani wetu wapo nafasi za chini katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema Minziro.

Kocha huyo alisema usajili walioufanya msimu huu utaleta ushindani ndani ya kikosi chake hicho na kudai malengo yake ni kushika nafasi tatu za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema anaridhishwa na viwango vinavyoonyeshwa na wachezaji wake nje na ndani ya uwanja jambo ambalo linampa matumaini ya kuendelea kuinoa timu yake hiyo na kuwataka mashabiki wake waendelee kuwapa ushirikiano.

Alisema ligi msimu huu ina ushindani mkubwa kila timu imejipanga kupata matokeo mazuri hivyo atapambana kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye michezo yao iliyobakia msimu huu ili atimize malengo yake.



Wachezaji wa mpira wa kikapu timu ya wenye ulemavu wakifanya mazoezi katika Viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *BMT yataka kalenda ya vyama vya michezo*

Na Shufaa Lyimo

BARAZA la Michezo Tanzania (BMT) limevitaka vyama vyote vya michezo kuwasilisha kalenda zao za mwaka 2023 ili wafahamu mikakati yao kiujumla ikiwamo mashindano wanayotarajia kuyafanya ndani ya mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano, Najaha Bakari, alisema hadi sasa ni vyama vitatu tu vilivyowasilisha kalenda zao ambavyo ni TABsa, Shimiwi pamoja na TBF.

Aidha alisema hilo ni agizo ambalo lilitolewa na Waziri mwenye dhamana ya michezo nchini, Mohamed Mchengerwa.

Wakati huo huo, Bakari alisema wanasikitishwa kuona mpaka sasa hakuna mgombea yeyote ambaye amejitokeza kuchukua fomu ya kuwania nafasi ya uongozi kwenye Chama cha Waandishi wa Habari za Michezo nchini (Taswa) ambapo uchaguzi wao unatarajiwa kufanyika Januari 28, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

"Tunasikitika hakuna mgombea yeyote aliyeonesha nia ya kuwania uongozi ndani ya chama hicho, tunasikia waandishi wengi wanakuwa wasemaji wazuri kwenye timu ama vyama vya michezo isipokuwa tunashangaa kuona hawahamasiki kugombea katika chama chao," alisema.

Alisema nafasi ambazo zinawaniwa ni Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Katibu Mkuu Msaidizi, Mweka Hazina, Mweka Hazina Msaidizi pamoja na wajumbe, ambapo aliweka wazi kuwa fomu za viongozi zinapatikana kwa Sh. 50,000.

## Ihefu sasa hasira zote kwa Prisons

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Ihefu FC, Zuberi Katwila, amesema mechi ijayo ataingia na mbinu mpya na silaha zake zote zilizosajiliwa kipindi cha dirisha dogo lililofungwa Januari 15, mwaka huu.

Ihefu FC imefanya usajili wa nyota wapya akiwamo Adam Adam aliyecheza mechi dhidi ya Yanga, Victor Akpan na Nelson Okwa wakitokea Simba na Yacouba Songne.

Nyota hao wanatarajia kuonekana kwenye mechi ijayo Ihefu itakapocheza na Prisons Jumamosi hii.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katwila alisema ameona madhaifu yaliyojitokeza katika mechi dhidi ya Yanga na kufanyia kazi haraka huku akitarajia kufanya mabadiliko katika kikosi chake kwenye mchezo huo dhidi ya Prisons.

Alisema mechi iliyopita na Yanga alifanya mabadiliko madogo safu ya ushambuliaji kwa kumwanzisha Adam na anatarajia mechi ijayo kikosi kuwa na mabadiliko makubwa.

"Mechi iliyopita na Yanga , tumefanya makosa na tunarudi uwanja wa mazoezi kufanyika kazi mapungufu yetu na kuboresha ubora tuliokuwa nao, nina matarajio mechi ijayo kutakuwa na mabadiliko ya kikosi na kuingia na mbinu tofauti na mechi iliyopita," alisema Katwila.

Alisema mabadiliko hayo ni kuhakikisha anawapa nafasi nyota wapya waliowasajili kipindi cha dirisha dogo ninaimani ni wachezaji wazuri na watasaidia timu kufikia malengo yetu ya kunusuru timu kutoshuka daraja.

Ihefu inashika nafasi ya 13 ya nne kutoka chini, ikiwa tayari imecheza mechi 20, imeshinda sita, sare mbili na amepoteza michezo 12 wakikusanya alama 20 katika msimamo wa ligi hiyo.

## Mbio za hisani kufanikisha matibabu wasioona

Na Mary Geofrey

NAIBU Spika, Mussa Zungu, amezipongeza klabu za Lions Club International District 411C Tanzania na Rotary E-Club kwa kuungana pamoja kufanikisha mbio za hisani, kwa ajili ya kukusanya fedha za kuendesha kambi za matibabu ya wagonjwa wa macho.

Naibu Spika aliyasema hayo wakati akihitimisha mbio hizo katika viwanja vya Farasi Oysterbay hivi karibuni jijini Dar es Salaam.

"Mbio hizi ni tukio muhimu sana kwa ajili ya kusaidia jamii, fedha itakayopatikana zitatumika kuendesha kambi za macho bure, kuwasaidia wananchi wetu wasiokuwa na uwezo kutibiwa bure, hongereni sana.

Wito wangu kwa kampuni nyingine binafsi ni kuendelea kuunga juhudi za Rais Suhulu Hassan katika kugusa maisha ya Mtanzania," alisema.

Naye Gavana wa Lions Club International District 411C Tanzania, Mustansir Gulamhussein amewashukuru wadau waliojitokeza kufanikisha mbio hizo za kimbia kwa ajili ya macho lengo likiwa kukusanya fedha kwa ajili ya matibabu ya macho.

"Lazima niwashukuru waliofika kuunga juhudi za Run for Sight, michango inayopatikana inaenda kusaidia wananchi wa Tanzania wanaohitaji huduma ya macho," alisema Mustansir Gulamhussein.

Naye Mwenyekiti wa Taasisi ya Lalji Foundation, Imtiaz Lalji, alisema kuwa matarajio ya tukio hilo ni kuwafikia zaidi ya watu 1,000 wenye matatizo ya macho.

"Malengo yetu ni kutoa michango kwenye sekta ya afya, elimu pamoja na kuwawezesha wajasiriamali kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania," alisema Imtiaz Lalji.

## ZISIKUPITE

### MAGUIRE ATAKIWA

KLABU ya West Ham inataka kumnunua beki wa kati wa England, Harry Maguire mwenye umri wa miaka 29 kwa mkopo kutoka Manchester United. (***Mirror***)

### GARNACHO AWINDWA

WINGA wa Manchester United, Alejandro Garnacho bado hajasaini mkataba mpya katika klabu hiyo ya Old Trafford, huku wawakilishi wa raia huyo wa Argentina wakitaka mshahara wa zaidi ya pauni 20,000 kwa wiki. Real Madrid na Juventus wanafuatilia hali ya kinda huyo mwenye umri wa miaka 18, ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2024 na ana chaguo la kuongezwa kwa mwaka mmoja. (***Independent***)

### DIABY AWANIWA ARSENAL

ARSENAL imefanya mawasiliano ya awali na Bayer Leverkusen kuhusu winga wa Ufaransa, Moussa Diaby lakini klabu hiyo ya Ujerumani haitaki kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 Januari hii. (Sky Sports)

### GUNDOGAN KUSAJILIWA BARCA

BARCELONA ina nia ya dhati ya kumsajili kiungo wa kati wa Ujerumani, Ilkay Gundogan kwa uhamisho wa bila malipo msimu wa joto wakati mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 na Manchester City utakapokamilika. (***Telegraph***)

### TROSSARD NA MUSTAKABALI

CHELSEA inafuatilia mustakabali wa fowadi wa Brighton, Leandro Trossard ambaye amekuwa akihusishwa na Arsenal na Tottenham Hotspur, huku Seagulls hao wakitarajiwa kupokea chini ya pauni milioni 25 kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 28. (Mirror)

### GONZALEZ APEWA OFA

KLABU ya Leicester City imetoa ofa ya pauni milioni 30 kumnunua mshambuliaji wa Argentina, Nicolas Gonzalez mwenye umri wa miaka 24 iliyokataliwa na klabu yake ya Fiorentina. (***90 Minutes***)

### JACKSON NA MKATABA

KLABU ya Southampton inakaribia kumpa mkataba wa kudumu mshambuliaji wa Senegal, Nicolas Jackson mwenye umri wa miaka 21, ambaye klabu yake ya Villarreal imetaja thamani yake kuwa ni euro milioni 20. (***Mail***)

### GALLAGHER KUREJESHWA

KLABU ya Crystal Palace ina nia ya kumrejesha kiungo wa kati wa Chelsea, Conor Gallagher katika klabu hiyo, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 22 akionesha kiwango kizuri wakati akicheza kwa mkopo huko. (***Sky Sports***)

### OUNAHI ATAKIWA NAPOLI

MKURUGENZI wa michezo wa Napoli, Cristiano Giuntoli amesema ana "matumaini" klabu inaweza kumsajili kiungo wa kati wa Angers na Morocco, Azzedine Ounahi mwenye umri wa miaka 22 ambaye amekuwa akihusishwa na Aston Villa na Leeds United. (***Sport Mediaset, kupitia Football Italia***)

### CARRASCO HUYO BARCA

WAKALA wa winga wa Ubelgiji, Yannick Carrasco amesema kuwa mazungumzo yanafanyika kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 kwenda Barcelona kutoka Atletico Madrid, huku fowadi wa Uholanzi Memphis Depay mwenye umri wa miaka 28 akielekea upande mwingine. (***Nieuwsblad***)

### BIELSA KUPEWA MEXICO

ALIYEKUWA kocha wa Leeds United, Marcelo Bielsa ndiye anayepewa nafasi kubwa zaidi na Shirikisho la Soka la Mexico kuchukua nafasi ya kuwa bosi wa timu ya taifa. (***ESPN***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BILIONEA ENGLAND AJITOSA KUINUNUA MANCHESTER UTD

### ●●● Awali aliitaka Chelsea, lakini akashindwa na sasa amepania...

**MANCHESTER,** England

KAMPUNI ya INEOS inayomilikiwa na bilionea, Jim Ratcliffe imeingia kwenye mchakato wa kuinunua Klabu ya Manchester United kutoka familia ya Glazer.

**Familia ya Glazers ili tangaza Novemba mwaka jana kuiweka sokoni Man United ili kuleta mabadliko.**

Mwanzoni kulikuwa na chaguzi ya kutafuta mwekezaji mpya katika klabu hiyo ya Ligi Kuu England au uwezekano wa "mauzo".

Malcolm Glazer alikamilisha ununuzi wa Man United ulioleta utata mwaka 2005, baada ya kununua hisa kwa mara ya kwanza Septemba 2003.

Ununuaji wake uliitumbukiza Man United kwenye deni kubwa kwa sababu mtaji mwingi uliotumika katika mkataba huo ulitokana na mikopo iliyopatikana dhidi ya mali ya klabu.

Familia ya Glazers ilikuwa haiungwi mkono na mashabiki wa klabu hiyo na sasa umiliki mpya unaonekana kukaribia.

Bilionea wa England, Ratcliffe ambaye ni shabiki wa Man United, alisajili nia hadharani Agosti mwaka jana baada ya kushindwa katika ombi la haraka la kuinunua Chelsea miezi mitatu iliyopita.

Ratcliffe mwenye umri wa miaka 70 anaonekana kulenga kuwa mbioni tangu mwanzo wakati huu, huku pia anamiliki klabu ya Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Nice.

"Tumejiweka katika mchakato huo," alisema msemaji wa INEO.

Ratcliffe ana utajiri wa dola bilioni 15.5 kwa mujibu wa jarida la Forbes, akiwa amejipatia utajiri wake mwingi tangu alipoanzisha kampuni kubwa ya kemikali ya INEOS mwaka 1998.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,067,6
MECHI KALI
AL-NASSR / AL HILAL
VERSUS
PARIS ST GERMAIN
1 | 6.53
X | 4.98
2 | 1.34
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ZIYECH SASA AWANIWA NEWCASTLE



**NEWCASTLE,** England

KLABU ya Newcastle imeripotiwa kupanga kuibomoa safu ya kiungo ya Chelsea kwa kulenga kuwasajili Hakim Ziyech, Conor Gallagher na Ruben Loftus-Cheek.

Gazeti la Telegraph limedai kuwa Ziyech yuko kwenye rada za kuondoka katika klabu hiyo ya London Magharibi ambayo imelazimika kuwaondoa wachezaji wawili kwenye kikosi chao cha Ligi ya Mabingwa Ulaya ili kusajili wapya.

Tayari kumekuwa na tetesi za uhamisho msimu huu wa baridi, lakini klabu hiyo ya Tyneside imeripotiwa kumhitaji zaidi kiungo wa kati kutokana na jeraha la Bruno Guimaraes.

The Blues wamekuwa wakitumia kiasi kikubwa cha fedha katika miezi ya hivi karibuni ili kuimarisha kikosi chao.

Wote wawili Gallagher na Loftus-Cheek wamekuwa hawana wakati mzuri chini ya kocha, Graham Potter msimu huu.

Kocha Potter anasemekana kuwa anamtaka Ziyech katika kipindi hiki cha dirisha la Januari, lakini anasitasita kuwaruhusu Gallagher au Loftus-Cheek kuondoka hapo Stamford Bridge.

# Suarez aanza na hat-trick Gremio



**RIO DE JANEIRO,** Brazil

LUIS Suarez aliifungia Gremio mabao matatu 'hat-trick' katika mechi yake ya kwanza katika kipindi cha kwanza na kuifanya timu yake mpya kutwaa ubingwa wa Recopa Gaucha.

Mshambuliaji huyo wa Uruguay alijiunga na klabu hiyo ya Brazil mwezi huu baada ya kuisaidia klabu yake ya utotoni, Nacional kushinda taji katika muda mfupi kabla ya Kombe la Dunia.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 aliahidi mabao alipokuwa akisaini mkataba wa miaka miwili na Gremio na bila shaka sasa mambo yameanza kuwa mazuri kwa upande wake.

Wakikabiliana na Sao Luiz katika mechi ya kombe la Recopa Jumanne, mabao matatu ya Suarez yaliipa timu hiyo ushindi wa 4-1 uliokamilika kabla ya mapumziko.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Suarez kufunga hat-trick kipindi cha kwanza kwa kipindi cha miaka 10, kwani kwa mara ya mwisho kufanya hivyo ni wakati akiwa Liverpool kwenye mchezo dhidi ya Norwich City, Desemba 2013.

## HABARI MICHEZO

# 15,605/-

# MKULIMA WA KALIUA ALAMBA MIL. 10/- JACKPOT BONUS

**Na Mwandishi Wetu**

MKULIMA wa mpunga kutoka Wilaya ya Kaliua Mkoa wa Tabora, Peter Andrew Dotto, ameshinda Sh. 10,681,562 katika Jackpot Bonus ya Sportpesa ya katikati ya wiki, baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya mechi 13.

Akizungumza kwenye hafla ya makabidhiano ya mfano wa hundi kwenye ofisi za Sportpesa, Dar es Salaam, Peter amesema alianza kucheza na Sportpesa mwaka 2019.

"Nilianza kucheza na Sportpesa miaka mitatu iliyopita baada ya kaka yangu mkubwa ambaye ni wa kwanza kushinda Sh. 600,000 wakati huo ilikuwa ni mwezi wa 12 na kimaisha kwa wakati ule tulikuwa tunapitia kipindi kigumu sana," alisema.

Kwa mujibu wa maelezo yake, Peter amesema tangu ameanza kucheza na Sportpesa amewahi kushinda mara tatu kabla ya ushindi huu na hiyo ilikuwa mwaka 2020.

"Nafikiri ilikuwa bahati yangu kwa wakati ule ambapo nilishinda Sh. 100,000, Sh. 70,000 na Sh. 190,000 kwenye hizi multibet," alisema.

Akielezea namna alivyopata ushindi huu wa Jackpot bonus ya kati kati ya wiki, Peter alisema kwanza yeye hana tabia ya kucheza kila siku au mara kwa mara, pili siku akiamua kucheza huwa anaweka mikeka si chini ya saba.

"Sijui kwa wengine lakini kwangu mimi sina kawaida ya kucheza kila siku ila huwa nikitaka kucheza najitahidi nichambue na kuweka japo mikeka ambayo haipungui saba. Ujue kabla sijashinda mkeka huu wiki moja nyuma niliweka mikeka kama 7 na mmoja wapo ulipata mechi 9.

"Rafiki yangu wa karibu naye aliweka mkeka kama mimi lakini yeye alishinda Jackpot bonus na kupata Sh. 300,000. Kitendo kile kilinitia hamasa ya kwa nini safari ijayo isiwe yangu. Nilichambua mikeka kwa umakini mkubwa na matokeo yake ndio unayaona haya nimeshinda Sh. 10,681,562".

Anaendelea kusema mkeka huu alioshinda aliuchambua kwa takriban siku 2 baada ya kuziona mechi za Jackpot siku ya Jumatatu.

Akimpongeza mshindi, Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Sportpesa, Sabrina Msuya, alimtaka kuendelea kucheza na Sportpesa na pia kuwafundisha wengine ambao bado wanasita kujisajili na Sportpesa ili na wao washinde kama yeye.




Mshindi wa Jackpot Bonus, Peter Andrew, kutoka Tabora akishikilia mfano wa hundi ya Sh. 10,681,562 baada ya kushinda Jackpot Bonus ya Sportpesa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtaiona Simba mpya - Oliveria

INATOKA UK 24

mchezaji mmoja mmoja na uwezo wake. Hii ni faida kubwa sana kwa upande wetu, sasa kila mtu akae tayari kushuhudia kile kilichotupeleka Dubai, lakini kikubwa maandalizi haya ni mechi za kimataifa, mtaiona Simba mpya, ya kipekee na iliyo bora," alisema Ahmed.

Meneja Habari na Mawasiliano huyo pia alisema haikuwa rahisi kwa CSKA Moscow kukubali mechi dhidi yao na kwanza kabisa ilibidi waiangalie timu wanayocheza nayo ikoje na itawapa nini kwenye mechi hiyo ya kujipima nguvu.

"Kwanza walitaka kujua ni timu ya namna gani, wakaambia kwao ni kawaida kufika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa kwa miaka ya karibuni. Halafu wakaambiwa kuwa ni ya 11 kwa ubora barani Afrika, baada ya hapo wakaenda kujidhihirisha wenyewe, hapo ndiyo wakakubali kucheza na sisi, vinginevyo wasingekubali na baada ya mechi wakakubali kweli ni timu nzuri," alisema. Naye straika Moses Phiri amesema amefurahi sana klabu yake kusajili mastraika wawili, Jean Baleke kutoka TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Mohamed Mussa kutoka KMKM ya Zanzibar kwa sababu itawapa nafasi ya kubadilishana na kupumzika.

"Ni vizuri sana, kwenye klabu huwezi kucheza peke yako, nimefurahia usajili kwa sababu mmoja anaweza kucheza na mwingine kupumzika na timu ikapata matokeo," alisema.

# Nabi aisuka upya safu ya ushambuliaji

INATOKA UK 24

Aliyesisitiza kuwaandaa kisaikolojia wachezaji wake zaidi kutokana na muda mchache wa mazoezi na mechi zilizopo mbele yao, baada ya kila siku nne kucheza mechi, hali hiyo benchi la ufundi kuhakikisha wanakuwa makini katika maandalizi ya kikosi chao.

Yanga inatarajiwa kushuka dimbani Jumamosi hii wakiwa nyumbani wakiwakaribisha Ruvu Shooting katika dimba la Benjamini Mkapa jijini Dar es Salaam saa 1:00 usiku.

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 21/01/23 | 18:00 | AFC Bournemouth vs Nottingham Forest | 2.60 | 3.20 | 2.65 |
| 02. 21/01/23 | 18:00 | Southampton FC vs Aston Villa | 2.80 | 3.30 | 2.42 |
| 03. 21/01/23 | 18:00 | Birmingham City vs Preston North End | 2.38 | 3.10 | 3.10 |
| 04. 21/01/23 | 18:00 | Blackpool vs Huddersfield Town | 2.27 | 3.15 | 3.20 |
| 05. 21/01/23 | 18:00 | Cardiff City vs Millwall FC | 2.95 | 3.05 | 2.48 |
| 06. 21/01/23 | 18:00 | Queens Park Rangers vs Swansea City | 2.55 | 3.25 | 2.70 |
| 07. 21/01/23 | 18:00 | Wigan Athletic vs Luton Town | 2.75 | 3.15 | 2.55 |
| 08. 21/01/23 | 18:15 | Espanyol Barcelona vs Real Betis Seville | 2.80 | 3.15 | 2.55 |
| 09. 21/01/23 | 22:00 | SC Cambuur vs Sparta Rotterdam | 2.95 | 3.35 | 2.31 |
| 10. 21/01/23 | 23:00 | RKC Waalwijk vs Go Ahead Eagles | 2.36 | 3.45 | 2.80 |
| 11. 22/01/23 | 13:30 | Gaziantep FK vs Sivasspor | 2.50 | 3.30 | 2.75 |
| 12. 22/01/23 | 15:00 | Sunderland AFC vs Middlesbrough FC | 2.80 | 3.25 | 2.45 |
| 13. 22/01/23 | 16:30 | Feyenoord Rotterdam vs Ajax Amsterdam | 2.85 | 3.55 | 2.28 |
| 14. 22/01/23 | 17:00 | Leeds United vs Brentford FC | 2.39 | 3.45 | 2.75 |
| 15. 22/01/23 | 17:00 | AC Monza vs Sassuolo Calcio | 2.26 | 3.30 | 3.10 |
| 16. 22/01/23 | 18:30 | Maritimo Madeira vs Estoril Praia | 2.55 | 3.15 | 2.80 |
| 17. 22/01/23 | 19:30 | Borussia Monchengladbac vs Bayer Leverkusen | 2.70 | 3.80 | 2.31 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 19/01/2023


| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2148 | Posta Rangers vs Kenya Police | 2.75 | 2.80 | 2.64 |
| 13:00 | 5527 | B 93 Copenhagen vs HB Koge | 3.58 | 3.99 | 1.75 |
| 13:30 | 4562 | Shahrdari Hamedan vs Esteghlal Khuzestan | 4.04 | 2.40 | 2.29 |
| 14:00 | 4819 | Kenkre FC vs Mohammedan SC | 5.58 | 3.82 | 1.52 |
| 14:30 | 1096 | MES Rafsanjan vs Nassaji Mazandaran | 1.93 | 3.01 | 4.00 |
| 14:30 | 5408 | Persis Solo vs Persija Jakarta | 2.89 | 2.79 | 2.52 |
| 14:30 | 5693 | Malavan Bandar Anzali vs Peykan FC | 2.33 | 2.64 | 3.42 |
| 15:15 | 1221 | Bidco United vs KK Homeboyz | 4.85 | 3.15 | 1.73 |
| 15:30 | 4616 | AL Adalh vs AL Baten | 2.12 | 3.30 | 3.40 |
| 15:45 | 5962 | Arab Contractors vs Aswan | 1.95 | 2.99 | 4.38 |
| 16:00 | 1357 | Sepahan Esfahan vs Esteghlal Tehran | 2.18 | 2.75 | 3.59 |
| 16:00 | 1365 | Africain vs ES Metlaoui | 1.56 | 3.27 | 6.64 |
| 16:00 | 1650 | EO Sidi Bouzid vs US Ben Guerdane | 2.07 | 3.05 | 3.46 |
| 16:00 | 2452 | US Monastir vs Olympique de Beja | 1.57 | 3.22 | 6.64 |
| 16:00 | 2873 | AS Slimane vs Avenir Rjich | 2.06 | 2.70 | 4.09 |
| 16:00 | 4958 | CSKA Moscow vs Gazovik Orenburg | 1.60 | 3.92 | 4.54 |
| 17:00 | 1192 | Atalanta vs Spezia | 1.42 | 4.54 | 6.54 |
| 17:00 | 4426 | Mumbai City FC vs Northeast United FC | 1.12 | 7.42 | 13.39 |
| 17:30 | 4275 | Gaziantep BB vs Konyaspor | 2.70 | 3.22 | 2.39 |
| 18:00 | 1128 | Olympique Safi vs Wydad Casablanca | 5.18 | 3.37 | 1.64 |
| 18:00 | 2428 | Thagafi Tulkarem vs Jabal EL Mokaber | 6.41 | 4.03 | 1.44 |
| 18:00 | 2607 | Gombe United FC vs Remo Stars | 1.84 | 3.00 | 4.45 |
| 18:00 | 2993 | Hilal Al-Quds vs Ahli AL Khalil | 1.34 | 4.57 | 7.47 |
| 18:00 | 3174 | Bodo Glimt vs Viking | 1.73 | 4.24 | 3.51 |
| 18:00 | 3632 | Shabab Al Dhahiriya vs Markez Balata | 2.33 | 3.11 | 2.85 |
| 18:00 | 5629 | National Bank vs El Ittihad Alexandria | 2.36 | 2.74 | 3.49 |
| 18:00 | 5666 | Al Ittihad Jeddah vs AL Faiha | 1.35 | 4.79 | 8.29 |
| 19:00 | 3700 | Iraq vs Oman | 1.96 | 2.70 | 4.56 |
| 20:00 | 1454 | MS Kiryat Gat W vs Hapoel Katamon Jerusalem W | 1.56 | 4.00 | 4.78 |
| 20:00 | 2719 | AS Tel Aviv University W vs Hapoel Nir Ramat Hasharon W | 2.26 | 3.69 | 2.59 |
| 20:00 | 2925 | Al-Nassr / AL Hilal vs Paris St Germain | 6.53 | 4.98 | 1.34 |
| 20:00 | 4478 | Hapoel Beer Sheva W vs Maccabi Bnot Emek Hefer W | 3.15 | 3.82 | 1.92 |
| 20:00 | 4519 | Pyramids vs Farco FC | 1.32 | 4.69 | 9.78 |
| 20:00 | 4697 | Lazio vs Bologna | 1.86 | 3.34 | 4.18 |
| 20:00 | 4818 | Anorthosis Famagusta vs EN Paralimni | 1.52 | 3.78 | 5.59 |
| 20:15 | 4699 | Maghreb Tetouan vs Olympique Khouribga | 2.27 | 2.64 | 3.57 |
| 20:30 | 2029 | Barcelona W vs Real Madrid W | 1.24 | 5.80 | 8.08 |
| 20:30 | 2294 | Fenerbahce vs Caykur Rizespor | 1.23 | 5.59 | 9.11 |
| 20:30 | 3241 | KAA Gent vs Charleroi | 1.57 | 4.09 | 5.19 |
| 22:00 | 1902 | Caruaru City PE vs Retro FC Brasil | 4.09 | 3.26 | 1.82 |
| 22:00 | 2341 | AD Ceuta vs Barcelona | 15.56 | 6.41 | 1.17 |
| 22:00 | 2752 | Ghana vs Sudan | 1.98 | 3.10 | 4.11 |
| 22:30 | 1204 | Sccm Chabab Mohammedia vs FUS Rabat | 4.85 | 3.15 | 1.73 |
| 22:45 | 2972 | St Truiden vs Brugge | 3.39 | 3.39 | 2.06 |
| 23:00 | 1837 | Manchester City vs Tottenham | 1.39 | 4.76 | 6.60 |
| 23:00 | 2638 | Juventus vs Monza | 1.63 | 3.69 | 5.26 |
| 23:00 | 5529 | Villarreal vs Real Madrid | 2.85 | 3.38 | 2.33 |

### IJUMAA - 20/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01:00 | 1091 | Peru U20 vs Brazil U20 | 13.55 | 5.42 | 1.19 |
| 01:00 | 4805 | Desportiva Alianca AL vs CRB AL | 7.26 | 3.47 | 1.48 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Nipashe
Alhamisi Januari 19, 2023



Bilionea England ajitosa kuinunua Man Utd UKURASA 21

# Mtaiona Simba mpya – Oliveria

●●● Atamba kocha huyo wa Brazil, asema siku saba alizokaa na kikosi kimebadilika na wachezaji wanamwelewa...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Roberto Oliveria, amewaambia wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kuwa watarajie kuiona timu yao ikiwa mpya na ya kipekee, huku Meneja Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally, akisema haikuwa rahisi kwa CSKA Moscow ya Urusi kukubali kucheza nao mechi, badala yake ubora wa viwango ndiyo uliosaidia.

Kocha huyo raia wa Brazil alisema kuwa amefurahi kuona kocha aliyemkuta Juma Mgunda ana ufundishaji wa soka kama la kwake, lakini sasa anachofanya ni kuingia falsafa nyingine mpya ili timu icheze soka la kisasa zaidi.

Akizungumza muda mfupi tu baada ya kutua kutoka Falme za Kiarabu ilikokwenda kupiga kambi kwa wiki moja, kocha huyo alisema pamoja na kwamba amekifundisha kikosi hicho kwa siku saba tu, lakini kimebadilika na kucheza soka safi na naamini muda unavyozidi kwenda mbele wachezaji wanaendelea kushika mafundisho yake.

"Nimefurahi sana kwa siku ambazo tulikuwa Dubai, tumefanya mazoezi na kucheza mechi mbili ikiwamo na timu kubwa duniani ya CSKA Moscow na wachezaji wetu walicheza vema sana hasa kipindi cha pili. Kutoka nao sare ya bao 2-2 na timu hiyo ya Urusi ni mafanikio makubwa kwa sababu si rahisi kutengeneza timu imara kwa muda wa siku tano tu," alisema kocha huyo.

Alisema kwa sasa anaendelea kuingiza falsafa mpya kwa vijana wake ili kutengeneza kikosi ambacho kitacheza soka la kisasa.

"Kaka yangu (Mgunda) na mimi tunafundisha soka linalofanana, lakini nataka niingize falsafa kwa wachezaji ili waweze kuboreka zaidi kwa kucheza soka la kisasa, nadhani mtashuhudia Simba tofauti na nzuri zaidi," alisema.

Kwa upande wa Ahmed alisema walikwenda Dubai ili kocha wao apate utulivu na usikivu zaidi kwa wachezaji wake aweze kuwafahamu.

"Tulihitaji kupata kambi yenye utulivu na usikivu ili mwalimu Robertinho aweze kuwaangalia vijana wake, kuangalia tabia ya

INAENDELEA UK 23




Roberto Oliveria

# Nabi aisuka upya safu ya ushambuliaji

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, ameweka wazi yupo makini kutengeneza upacha kati ya mshambuliaji mpya, Kennedy Musonda pamoja na kinara wa mabao wa timu hiyo, Fiston Mayele ili kuwa na muunganiko mzuri na kuimarisha safu hiyo.

Nabi alimtumia Musonda katika mechi na Ihefu FC kwa kuchezesha washambuliaji watatu akiwamo Mayele aliyeanza tangu dakika ya kwanza pamoja na kumwingia Clement Mzize na kufanikiwa Yanga kupata ushindi wa bao 1-0 katika mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Nabi alisema anaimani na uwezo wa Musonda, anafanyia kazi maigizo mapya ya wachezaji kutengeneza muunganiko mzuri huku akihitaji kutengeneza pacha imara kati ya nyota huyo na Mayele ili kuwa tishio safu ya ushambuliaji.

Alisema kuna mabadiliko makubwa ya wachezaji kuondoka na kuingia, inayomlazimu kuwa makini katika kuhakikisha anakuwa na muunganiko mzuri kwa wale wapya na wazamani.

"Kulingana na usajili uliofanywa, nitabadilisha mfumo kutokaa na wachezaji niliokuwa nao. Musonda ni mchezaji mzuri na naendelea kuwatengeneza kuhakikisha wanakuwa vizuri kucheza na Mayele," alisema.

Mpira ni mchezo wa muunganiko na kila mmoja anatakiwa kuwa sawa na mwenzake kujituma katika uwanja wa mazoezi na kuvihamisha katika mechi, sina mashaka na Musonda kwa sababu anahitaji muda wa kuzoea," aliongeza .

Alisema anahitaji kuona wachezaji wake wanakuwa makini na kujitolea katika kutafuta pointi tatu katika kila mechi kwa sababu ya ugumu wa ligi hasa hatua hii ya lala salama.

"Naongea na wachezaji wangu kuhusu ugumu wa ligi msimu huu na kuhakikisha kila mechi kwetu tunaingia kama fainali, hatutaki kupoteza pointi kwa sababu ya kuwahofia wapinzani wetu ambao wanaotofautia katika msimamo," alisema kocha huyo.

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >